SportPesa
TZS. 761,374,640
NI YA KWAKO WIKI HII, BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 3

**MWANAKIJIJI** agundua madini ya dhahabu wakati akichimba choo




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Desemba 11, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580791

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# MWENDO WA SHANGWE

**VIKWAZO** 46 Tanzania na Kenya vyatatuliwa, Samia ataka kulipa mahari kupata faru majike, Kenyatta aomba ndege korongo... *Endelea ukurasa wa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na mgeni wake, Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 3

## AHUKUMIWA KUNYONGWA HADI KUFA KWA KUMUUA BIBI KIZEE

Mkazi wa Kijiji cha Genkuru, tarafa ya Ingwe, Tarime mkoani Mara, Buriani Chacha, amehukumiwa kunyongwa hadi kufa baada ya kupatikana na hatia...

UKURASA WA 4

## WATOROKA MASOMO WAKATI WA HEDHI

UKOSEFU wa walimu wa kike katika shule ya sekondari Mapanda katika halmashauri ya Ushetu, Kahama mkoani Shinyanga, umesababisha wanafunzi wa kike kushindwa kupata mtu wa kumweleza shida zao wanapokuwa kwenye hedhi.
Hatua hiyo huwafanya...

# Polisi amtwanga risasi mwenzake wakiwa lindoni



UKURASA 2

## WHO yataka hadhari corona msimu sikukuu

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA, YANGA 'KITAUMANA' UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Polisi amtwanga mwenzake risasi lindoni

**Na Said Hamdani,** LINDI

Polisi mwenye cheo cha Konstebo, Onesmo Joseph, amekufa baada ya kupigwa risasi na askari mwenzake, aliyetajwa kwa jina la Joseph, walipokuwa wanalinda Benki ya CRDB Tawi la Ruangwa.

Habari za kutoka wilayani humo zilizothibitishwa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna Msaidizi (ACP) Mtatiro Kitinkwi, zimeeleza kuwa mauaji hayo yalifanyika juzi saa 6:30 mchana.

Kitinkwi amesema siku ya tukio, askari hao wakiwa lindoni, kulitokea mtafaruku baina yao ndipo Konstebo Joseph akampiga mwenzake risasi sehemu ya nyonga ya mguu wa kulia na kumsababishia maumivu makali.

Alisema chanzo cha ugomvi kilichosababisha askari hao hadi wapigane risasi bado hakijafahamika mara moja lakini baadhi ya watu wanadai walikuwa wanagombea mwanamke, huku wengine, akiwamo Kamanda Kitinkwi, wakidai unatokana na pikipiki.

"Mpaka sasa chanzo cha uhakika kuhusu ugomvi wao bado hakijafahamika licha ya kuwapo taarifa kwamba unatokana na mtuhumiwa kuchelewesha kurejesha pikipiki ya marehemu aliyokuwa ameazima," alisema Kitinkwi.

Kamanda Kitinkwi alisema Onesmo alifariki dunia akiwa njiani kupelekwa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dar es Salaam kwa ajili ya kuendelea na matibabu.

Aidha, Kitinkwi amesema Konstebo Joseph tayari amefukuzwa kazi na sasa anaandaliwa utaratibu wa kufikishwa mahakamani kujibu shitaka la mauaji linalomkabili dhidi ya mwenzake akiwa raia.

"Hatua za awali askari huyu (mtuhumiwa) tumemfukuza kazi kwa kutenda kosa la jinai," alisema Kitinkwi.

# TRA yayanasa malori ukaguzi risiti za EFD

**Na Mwandishi Wetu,** MKURANGA

MAMLAKA ya Mapato (TRA) imefanya ukaguzi wa risiti za kielektroniki (EFD) katika malori ya mizigo wilayani Mkuranga mkoani Pwani na kubaini kuwapo tatizo la kikodi katika mizigo hiyo.

Watumishi wa mamlaka hiyo jana walifanya ukaguzi wa risiti hizo katika malori ya mizigo yanayoelekea mikoa ya kusini kwenye eneo la Mwandege wilayani Mkuranga na kubaini dosari hizo.

Ukaguzi huo ulianza Desemba 8 mwaka huu.

Katika ukaguzi huo jana, magari 21 yalikutwa na makosa kwa mujibu wa maofisa wa TRA walioshiriki katika ukaguzi huo.

Meneja Msaidizi wa Mkoa wa Pwani wa TRA, Omar Chikwekwe, alisema wenye malori hayo wanavizia muda wa usiku kwa kuamini kuwa TRA muda wao wa kazi umeisha, hivyo ni rahisi kwao kupitisha mizigo.

Aliwahimiza wafanyabiashara wenye malori, wenye viwanda na wafanyabiashara wanaouza bidhaa, kutokukwepa kutoa risiti kwa manufaa ya taifa.

Alisema ukaguzi unaendelea katika njia kuu zote zitokazo Dar es Salaam pamoja na Kariakoo.




Balozi wa Canada hapa nchini, Pamela O'Donnell (kulia), akiwa na zawadi aliyokabidhiwa na Mwenyekiti wa Mtandao wa Elimu Kairuki (KHEN), Kokushubira Kairuki (katikati) na Makamu Mkuu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU), Prof. Charles Mgone (kushoto), wakati wa kongamano la kitaaluma la chuo hicho, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mwendo wa shangwe Tanzania, Kenya

**Na Romana Mallya**

NI mwendo wa shangwe! Ndivyo ambavyo unaweza kusema kutokana na Rais Uhuru Kenyatta na mwenyeji wake, Rais Samia Suluhu Hassan kukubaliana kumaliza vikwazo 18 vya kibiashara vilivyobaki kati ya Tanzania na Kenya.

Viongozi hao wamesema awali kulikuwa na vikwazo 64 baina ya mataifa hayo, lakini mazungumzo ya hivi karibuni baina yao yameondoa vikwazo 46.

Rais Samia aliyasema hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam wakati wa utiaji saini makubaliano ya ushirikiano kati ya Tanzania na Kenya.

"Tulipokutana wakati ule tulikuwa na vikwazo vingi, 64 vya biashara lakini tukasema kwa kutumia majina yetu, tukasema Uhuru wa kufanya biashara Kenya au Tanzania na Suluhu tulikubaliana tufute matatizo yanayotukabili.

"Tukatumia majina tukaondoa vikwazo 46 kati ya 64, faida yake ni kwamba kuna ukuaji wa biashara, tumetoka Sh. bilioni 885 hadi na Sh. trilioni 1.1," alisema.

Rais Samia alisema kuwa katika uagizaji bidhaa, Kenya iliziagiza kutoka Tanzania zaidi ya mara tatu kulinganishwa na mwaka uliopita na upande wa Tanzania iliuza bidhaa zenye thamani hiyo.

Alisema wamebaini bado kuna matatizo na wamekubaliana mawaziri wa pande zote mbili waendelee kukutana na kuona vile vilivyobaki kama ni kubadilisha sera au sheria waviondoe ili biashara iendelee kukua.

"Tulipokutana Nairobi tulisema tume zetu za ushirikiano ziendelee kukutana na mwezi Agosti walikutana na kuna mambo mengi wameyafanyia kazi na tumekubaliana, ndiyo maana leo (jana) tumesaini mikataba hii," alisema.

Rais Samia alibainisha kuwa katika mkutano huo, pia walijadili masuala mbalimbali katika maeneo ya siasa na diplomasia, ulinzi na usalama pamoja na miradi ya pamoja ya miundombinu na uchukuzi.

Mkuu wa Nchi huyo alisema punde wataweka mawe ya msingi baada ya kukubaliana katika miradi mikubwa ya miundombinu ambayo ni barabara, bandari na nishati.

Pia alisema wamekubaliana kuendelea kuimarisha mipaka na wamewaachia kazi hiyo mawaziri wanaohusika wakalimalizie kutia saini ili washerehekee.

**UVIKO-19**

Rais Samia alisema wamekubaliana kushirikiana katika mapambano dhidi ya UVIKO-19 kwa kuwaelekeza mawaziri wa afya ambao wametia saini kwenda kulishughulikia kwa sababu wote ni waathirika.

"Sote tumepokea maradhi haya lakini wote tunafungiwa na kunyimwa haki na pengine kutembea nje au watu kuwekewa mipaka kuja kwetu," alisema.

**NDOA YA FARU**

Rais Samia pia alibainisha kuwa miongoni mwa maeneo ya kushirikiana ni sekta ya utalii kwa sababu ikolojia ya nchi hizo inafanana, hivyo wamewaagiza mawaziri wa sekta hiyo kuondoa vikwazo ili mataifa hayo kila moja lifaidike kwa kuleta watalii zaidi na kupata mapato mengi.

Alisema huko nyuma, Kenya walikuwa wanaona ndege aina ya korongo wako Tanzania na wao hawana hivyo inabidi mtalii aje huku kuwaona.

"Ndugu zetu waliomba na leo nina furaha kumkabidhi Mheshimiwa Rais cheti maalumu cha ndege hawa 20 ambao tunawapeleka Kenya ili wakae kwenye mbuga za wenzetu. Tanzania ina korongo 4,000 na Kenya inao 12 tu, taratibu zikitimia watafika kabla ya Krismasi, iwe ndiyo zawadi yetu ya Krismasi kutoka Tanzania kwenda Kenya.

"Nami nikatumia fursa hapo hapo, nikamwambia kwenye mbuga zangu kule Ngorongoro pengine na Serengeti nina madume wawili tu wa faru hawana wake, hawana wenza, nikawaambia siyo vibaya hawa faru wakioa Kenya, tupo tayari kutoa mahari, tupate faru majike waolewe Tanzania, mdogo wangu amenikubalia. Siku ya kuwapokea lazima tukate keki ya hiyo ndoa ya faru hao," alisema.

**BOMBA LA GESI**

Kuhusu mradi wa bomba la gesi kutoka Tanzania kwenda Kenya, Rais Samia alisema wamewaachia mawaziri wa nishati walishughulie ikiwamo mradi wa gesi ya majumbani.

Aliwataka mawaziri na maofisa wa nchi hizo mbili kuwa hivyo ndiyo wanavyotakiwa kwenda ili mataifa hayo yawe na nguvu ya kiuchumi.

Pia alisema wamekubaliana kutafutwe siku ya kuweka mawe ya msingi kwenye ujenzi wa barabara (Magamoyo-Malindi) na wataunganisha eneo la Pwani.

Alisema jambo lingine walilokubaliana ni kushirikiana kukabiliana na vitendo vya uhalifu vinavyovuka mipaka ikiwamo ugaidi, biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu na dawa za kulevya.

Alitaja eneo lingine walilokubaliana ni kuanza kuelekea katika mambo ya uchumi na kuimarisha uhusiano.

"Tunaudhiana, tunaviambiana kisha tunaambizana hebu njoo tukae kwani kitu gani, si wewe uliniambia hivi... aah! hiyo tu aah! iishe bwana na tunaendelea, hiyo ndiyo Kenya na Tanzania," alisisitiza.

Kenyata aliwashukuru Watanzania kwa kumwalika kusherehekea maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru, akibainisha kuwa yeye na Tanzania ni rika moja, akikumbusha kuwa miaka 60 iliyopita baba yake alikuja kwa sherehe hiyo.

Pia aliishukuru serikali kwa kumpatia zawadi ya ndege ambao watasaidia kukuza utalii wao na kumhakikisha nao watatoa faru weusi.

"Na hiyo harusi uliyosema tutatafuta siku ya kuja kukata keki pamoja na ndiyo pia waweze kuongezeka upande wa Tanzania na pia tutatafuta siku ya kuja kukutane kufungua mpaka," alisema.

**HABARI KITAIFA**

# Ahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa kumuua bibi kizee

**Na Samson Chacha,** TARIME

MKAZI wa Kijiji cha Genkuru, tarafa ya Ingwe, Tarime mkoani Mara, Buriani Chacha, amehukumiwa kunyongwa hadi kufa baada ya kupatikana na hatia ya mauaji.

Chacha (32) amehukumiwa baada ya kubainika kumuua Mugosi Nyagana (73) kwa kumpiga na jiwe kichwani sehemu za kisogoni akimtuhumu kuwa ni mchawi kisha kwenda kutupa mwili wake kichakani jirani na nyumba yake.

Mshtakiwa alisomewa hukumu hiyo juzi mbele ya Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Musoma, John Kahyoza, katika kikao cha Mahakama hiyo kilichoketi na kuendelea na kesi wilayani Tarime.

Jaji Kahyoza alisema ushahidi uliotolewa katika kesi hiyo ya mauaji, umethibitisha bila kuacha shaka kuwa mtuhumiwa alikuwa na nia ovu ya kufanya mauaji.

"Kama ulivyoshtakiwa, mahakama hii inakuhukumu kunyong'wa hadi kufa ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye nia ya kuwadhuru wenzao na kupoteza nguvu kazi kwa familia iliyoathirika na taifa kwa ujumla," alisema Jaji Kahyoza.

Awali, Mwanasheria wa Serikali, Yese Temba, alidai mahakamani hapo kuwa mtuhumiwa alifanya mauaji hayo Aprili 18, 2018 saa 12:00 jioni katika Kijiji cha Genkuru kwa kumpiga kwa kutumia jiwe kichwani sehemu za kisogoni Mugosi Nyagana.

Temba alidai kuwa kitendo hicho kilisababisha kutokwa damu nyingi na kuharibu mfumo wa ubongo na kusababisha kifo chake.

Baada ya kufanya kitendo hicho, alidai kuwa aliuchukua mwili wa marehemu na kwenda kuutupa vichakani na kukutwa na wananchi na familia ya marehemu.

"Chanzo cha mauaji hayo ya kujichukulia sheria mkononi ni kutokana na mshitakiwa kumtuhumu Nyagana kuwa ni mchawi anaroga familia yake na mashamba yake.

Katika kesi hiyo, upande wa mashitaka ulipeleka mahakamani mashahidi wanne walioshuhudia tukio hilo wakiwamo wajukuu wa shangazi wa Nyagana na fomu namba tatu (PF3) uchunguzi wa daktari.

Kabla ya kutolewa hukumu, mshtakiwa alipewa nafasi ya kujitetea na kudai kuwa walikuwa na mgogoro wa mahari ya ndugu yao aliyeolewa na ndoa kuvurugika hivyo kutaka mahari irejeshwe hali iliyosababisha chuki na yeye mtuhumiwa kuchomewa mji wake na kuhamia Nyamongo, hivyo kuiomba mahakama imsamehe.

# WHO yataka Watanzania wachukue hadhari corona

**Na Romana Mallya**

MWAKILISHI Mkazi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Tanzania, Dk. Tigest Mengestu, amewataka Watanzania kuendelea kuchukua tahadhari kwa kuwa ugonjwa wa UVIKO-19 bado upo.

Alitoa angalizo hilo jana wakati ambao Watanzania na mataifa mengine duniani kwa sasa yapo katika maandalizi ya sikukuu za mwisho wa mwaka ambazo hukutanisha watu.

Dk. Mengestu alitoa tahadhari hiyo jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu umuhimu wa afya kwa wote nchini.

Aliwataka Watanzania kuchukua tahadhari zote ikiwa ni pamoja na kuchanja ili kujiweka imara zaidi dhidi ya virusi vya corona.

Akizungumzia taarifa za baadhi ya nchi kuwekewa vikwazo kutokana na ugonjwa huo, ofisa anayehusika na masuala ya majanga na dharura, Dk. Grace Saguti, alisema shirika linaelekeza watu waendelee kufanya kazi kwa kuzingatia maelekezo ya watalaamu na hakuna nchi inatakiwa kuiwekea nchi nyingine vikwazo.




Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Wafanyabiashara Wanawake (TWCC), Mwajuma Hamza (kulia), akiwaaga wanachama 36 wa chama hicho, wanaokwenda Dubai kushiriki maonyesho ya Dubai Expo 2020, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Agundua dhahabu akichimba shimo la choo

**Na Mohab Dominick,** MBOGWE

MKAZI wa kijiji cha Kakumbi, Mbogwe mkoani Geita, Said Tangawizi, amegundua madini ya dhahabu wakati akichimba shimo la choo kwenye eneo lake la uwekezaji wa ghala la kuhifadhia mazao.

Kutokana na ugunduzi huo, amefanya maridhiano kupitia mkutano wa serikali ya kijiji ili kubadili eneo hilo lenye makazi ya watu kuwa la uchimbaji.

Baada ya mkutano huo, Tangawizi alisema neema hiyo ilitokea juzi wakati vibarua aliowatuma kuchimba shimo la choo, kukutana na mwamba unaosadikiwa kuwa na madini ya dhahabu na alipoyachukua kwa lengo la kuyapima kiasili (chabo) mawe hayo yalionekana kuwa na dhahabu nyingi.

"Baada ya kupatikana dhahabu kwenye shimo la choo, kwa kweli nilichukua hatua ya kuieleza serikali ya kijiji kupitia ofisa mtendaji wa kata na baadaye diwani ambaye alipeleka taarifa hizi ofisi ya madini ili kupata utaratibu maalumu," alisema Tangawizi.

Pia alisema licha ya wananchi kukubaliana kuchimba dhahabu kwenye eneo hilo, binafsi aliridhia kwa kutambua kuwa sheria ya madini inatamka wazi kuwa madini ni mali ya serikali hata yangetokea maeneo tata.

Diwani wa Lugunga, Enock Magulu, alisema alipata taarifa hizo kupitia ofisa mtendaji wa kata na alipofuatilia zaidi ofisi za madini walimtaka athibitishe madai hayo, alifika kwenye eneo hilo na kuruhusu kuchimbwa kwa maduara manne na kujiridhisha kuwa kuna madini ya dhahabu.

"Baada ya hapo serikali ya kijiji iliitisha mkutano wa hadhara wa waanchi ili kupata maoni yao na kupitia mkutano huo waliridhia eneo la kijiji chao lichimbwe madini hayo ili wapate maendeleo," alisema Tangawizi.

Wakazi wa kijiji hicho, Pendo John na Ntemi Mtoka, wameiomba serikiali kuruhusu eneo hilo lichimbwe kwa kuwa wao wenyewe wameridhia kupitia mkutano wa hadhara eneo hilo lichimbwe kusitokee pingamizi lolote.

"Tuwakumbushe tu viongozi kuwa sisi tupo tayari kutumia fursa ya rasilimali hii iliyopatikana kijijini kwetu kwamba tuitumie kupata maendeleo yetu na kijiji kwa ujumla. Lakini kutokana na mlipuko huu kuibukia kwenye makazi ya watu, wakumbuke suala la kuhifadhi mazingira maana umati wa watu utakuwa mkubwa," alisema Mtoka.

Kaimu Mwenyekiti wa kijiji hicho, ambaye pia ni Mwenyekiti wa kitongoji cha Kakumbi, Jonathan Mahega, alithibitisha kutokea kwa ugunduzi wa madini hayo na kwamba serikali ya kijiji kupitia mkutano halali uliofanyika kijijini hapo, kwa pamoja walikubaliana kubadili matumizi ya ardhi na kuwa ya uchimbaji.



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (wa tatu kulia), akishuhudia utiaji saini mikataba ya ununuzi wa bomba na pampu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji kupitia mpango wa maendeleo wa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya Uviko-19 kati ya Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Clement Kivegalo (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji Helpdesk Engineering Tanzania Ltd, Annadurai Krishnasamy, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## RIPOTI MAALUMU -2
# Neema ya mgodi inapogeuka shubiri

**KATIKA toleo la jana, mkazi wa Kitongoji cha Kigonga B, Kijiji cha Matongo, Kata ya Matongo wilayani Tarime, Sadock Maningo (48), alieleza namna alivyokataa kupokea Sh. milioni 62.905 ili makazi yake yabomolewe kupisha upanuzi wa mgodi wa dhahabu wa Nyamongo, maarufu Barrick North Mara.**

**Vilevile, ilielezwa namna wakazi wa kitongoji cha Nyamichere, kijiji cha Nyakunguru, wanavyosubiri fidia ya kupisha upanuzi wa mgodi huo kwa miaka tisa sasa pasi na dalili za mafanikio. Endelea kufuatilia ripoti hii kujua mustakabali wake.**

### HATUA ZA DIWANI

Kimsingi wajibu mkuu wa diwani ni kutetea maslahi ya wananchi kwenye eneo analoliwakilisha. Vipi kuhusu wawakilishi wa wakazi wa wanaozunguka mgodi wa dhahabu wa Nyamongo?

Diwani wa Viti Maalum tarafa ya Ingwe, Eliza Malembera, anasema amefuatilia suala la fidia kwa wananchi wake na kupatiwa mrejesho kwamba uongozi wa mgodi umeamua kuachana na mpango wa kutwaa maeneo hayo, hivyo yatabaki kuwa mali ya wananchi.

"Sasa unajiuliza hawa wananchi wamezuiwa kufanya shughuli za maendeleo kwenye maeneo yao toka mwaka 2012, leo unawaambia huna mpango na maeneo yao tena. Hii ni haki kweli?

"Tumelifikisha suala hili kwenye vikao vya Baraza la Madiwani lakini bado kimya kimetawala japo alifika mmoja wa maofisa wa mgodi kwenye moja ya vikao vyetu akasema eneo hili hawalihitaji tena.

"Aliahidi kuwa watalipa fidia kidogo ya usumbufu. Waliahidi kuwa ingelipwa Septemba mwaka huu lakini hadi sasa (Novemba 21, 2021) hakuna kilicholipwa kwa wananchi.

"Ukweli ni kwamba wananchi wamepata hasara kubwa kutokana na kusimamishwa kuendeleza maeneo yao kwa kipindi chote hicho cha miaka tisa," anasema.

Kuhusu Maningo, diwani huyo anatoa pongezi kwa mkazi huyo wa kijiji cha Matongo kuweka nadhiri ya kutoachia eneo lake hadi pale atakapolipwa fidia stahiki.

### WADAU HAKI NA SHERIA

Mratibu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) Ofisi ya Arusha, Wakili Hamisi Mayombo, anasema wanafuatilia kwa karibu yanayoendelea Nyamongo.

Wakili Mayombo anasema kwamba baada ya kufuatilia suala la Maningo, kituo chao kinaona mwananchi huyo anastahili kulipwa Sh. milioni 129.354 ya fidia ya mali zake ili kupisha upanuzi wa mgodi na si vinginevyo.

"Kuhusu wakazi wa kitongoji cha Nyamichere, LHRC tumeamua kuwasaidia kufungua shauri mahakamani ili kudai haki yao ya fidia.

"Tumeona kuna shida mgodi kuzuia shughuli za maendeleo kwenye maeneo yao halafu baada ya miaka tisa uongozi wa mgodi useme hauna mpango na maeneo hayo. Hii siyo sawa, siyo haki," Wakili Mayombo anasema.

### KAULI YA BARRICK

Nipashe inatua mezani kwa Ofisa Uhusiano wa Barrick North Mara, Gilbert Mworia, ambaye anakiri bado hawajamlipa fidia Maningo kutokana na mkazi huyo wa kijiji cha Matongo kukataa kutia saini nyaraka za malipo zilizoandaliwa.

"Sisi (Barrick North Mara) tuko tayari kumlipa hata leo. Shida ni kwamba kwa sasa tunatumia maofisa wa serikali kufanya tathmini ya maeneo yote tunakohitajika kulipa fidia.

"Sasa nyaraka za kumlipa huyo jamaa (Maningo) tulizopewa zinasema alipwe Sh. milioni 83. Tukimlipa zaidi ya hapo tutaingia kwenye makosa ya utakatishaji.

"Hapo anapoishi ni karibu sana na mgodi, ni hatari kiusalama. Tutakwenda kuzungumza naye tena ili akubali kulipwa fidia aondoke kwenye eneo hilo," anasema.

Kuhusu wakazi wa Nyamichere, Mworia anasema wameamua kutoyatwaa maeneo yao kwa kuwa mgodi umebadili mpango wa uchimbaji.

"Kwa kuwa maeneo yale yamekaa kwa muda mrefu bila kuendelezwa, wamiliki wake watalipwa kifuta jasho, lakini lazima tufanye uhakiki kwanza maana huku kuna ujanja ujanja mwingi sana linapokuja suala la kulipa fidia," Mworia anasema.

### MKUTANO WA MBUNGE

Mei Mosi mwaka huu, Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara (CCM), alizungumza na wananchi kijijini Nyakunguru ambako wananchi wanasubiri kulipwa fidia za mali kwa miaka tisa sasa tangu maeneo yao yalipofanyiwa tathmini na kuzuiwa kuyatumia kwa shughuli yoyote.

Waitara ambaye pia ni Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, alisema siku hiyo kuwa wananchi hao wakae mkao wa kula kwa kuwa alikuwa na taarifa kutoka serikalini kwamba mpango wa kuwalipa ungeanza kutekelezwa wiki ya kwanza ya Mei mwaka huu, jambo ambali halijafanyika hadi sasa.

### USULI NA HISTORIA

Ikirejewa historia ya uchimbaji dhahabu Tanzania, inaanzia mwaka 1894 dhahabu ilipoonekana maeneo ya Kanda ya Ziwa. Mgodi wa kwanza wa dhahabu nchini ni Sekenke ulioanza mwaka 1909.

Mgodi wa dhahabu North Mara ulifunguliwa rasmi mwaka 2002. Ilipotimu mwaka 2014, ilikadiriwa kuwa uhai wa mgodi huo utakoma miaka tisa baadaye, yaani kufikia mwaka 2023.

# Watoroka masomo wakati wa hedhi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

UKOSEFU wa walimu wa kike katika shule ya sekondari Mapanda katika halmashauri ya Ushetu, Kahama mkoani Shinyanga, umesababisha wanafunzi wa kike kushindwa kupata mtu wa kumweleza shida zao wanapokuwa kwenye hedhi.

Hatua hiyo huwafanya watoroke masomo bila kuomba ruhusa mpaka wanapomaliza kipindi hicho.

Hayo yalibainishwa jana wilayani hapa na baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo wakati wakizungumza na mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, aliyetembelea shule hiyo kukagua utekelezaji wa ujenzi wa vyumba vya madarasa na kusikiliza shida mbalimbali zinazowakabili wanafunzi hao.

Mmoja wa wanafunzi hao, Pendo Michael, anayesoma kidato cha tatu, alisema shule yao ina walimu saba wote wa kiume hali ambayo inawafanya washindwe kueleza shida zao hususani wakati wa hedhi.

Kutokana na hali hiyo, alimuomba mbunge huyo kusaidia wapate mwalimu wa kike ili wawe wanamweleza shida zao wanapokuwa katika kipindi hicho.

Mwanafunzi mwingine, Mericiana Kimisha, alisema wakati wanapokuwa katika siku zao za hedhi wanashindwa kuwaeleza walimu wa kiume kwa kuona aibu na badala yake wamekuwa wakisingizia kuwa wanaumwa ili kupata muda wa kwenda nyumbani.

"Sisi wasichana tuna changamoto nyingi. Tunaomba serikali isikilize kilio chetu cha muda mrefu. Baadhi yetu tumekuwa tukifanyiwa ukatili na wazazi pamoja na walezi lakini kusema matatizo hayo kwa walimu wa kiume imekuwa changamoto kwetu," alisema Kimisha.

Diwani wa Mapamba, Yohana Mange, alisema tayari kero hiyo alishaiwasilisha kwa Mkurugenzi wa halmashauri hiyo na kuahidiwa kupatiwa mwalimu mmoja wa kike lakini utekelezaji wake bado haujafanyika mpaka sasa.

Mkuu wa Shule hiyo, Lau Singasinga, alisema shule hiyo ina walimu saba na wanafunzi 150 ,wasichana wakiwa ni 74.

Alisema wanafunzi wa kike wanahitaji kupata mwalimu wa kike kwa ajili ya malezi yao na kwamba walimu wa kiume ni vigumu kuwaeleza shida zao.

Mbunge huyo alimuomba Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Lino Mwageni, kutatua kero hiyo kwa kuwa suala hilo liko ndani ya uwezo wake ili kuondoa kero hiyo ambayo imedumu kwa muda mrefu.

Aliwataka maofisa elimu kuhakikisha wanazitembelea shule zilizopo pembezoni ili wakatatue shida mbalimbali zinazowakabili wanafunzi hususani wa kike.

## TANGAZO

# NOTISI/TANGAZO

MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, NGOMENI AUCTION MART,MOPEH COMPANY LTD,KOTI BROTHERS LTD,MBUZAX AUCTION MART kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| UBUNGO | DOREEN JAMES TEMBA | NYUMBA | DOREEN JAMES TEMBA | GONGO LA MBOTO | 03/01/2022 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | ERNEST JOHN MSHUBI | NYUMBA | ERNEST JOHN MSHUBI | SALA SALA | 30/12/2021 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | HUSSEIN KAMANA SAID | NYUMBA | HUSSEIN KAMANA SAID | CHAMAZI | 02/01/2022 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | HAYSAM HAMADA YAHAYA | NYUMBA | HAMADA YAHAYA HAMISI | KISASA | 02/01/2022 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | ALFRED MULLISA GOSBERT | NYUMBA | ALFRED MULLISA GOSBERT | BUNJU A | 03/01/2022 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | ANNA PIUS DAMIAN | NYUMBA | INNOCENT BENARD | MBEZI JUU | 29/12//2021 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | MARY MICHAEL MLAPONI | NYUMBA | MARY MICHAEL MLAPONI | YOMBO DOVYA | 28/12/2021 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | JUMA OMARY SADALA | NYUMBA | JUMA OMARY SADALA | GOGO ZINGIZIWA CHANIKA | 28/12/2021 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | THECLA HERBERT MASANJA | NYUMBA | GODWIN ELIAMEN SEIYA | MAPINGA | 27/12/2021 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | HUSAM SEA FOOD | NYUMBA | ALLY SAIDI MNENDE | MBAGALA KUU MASHARIKI | 28/12/2021 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | GOTHELFU JOSHUA NNKO | NYUMBA | GOTHELFU JOSHUA NNKO | BOMANG'OMBE | 28/12/2021 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | PIUS KARIMU CALIST | NYUMBA | PIUS KARIMU CALIST | BONITE | 29/12/2021 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | JAMILA KONDO GEMA | NYUMBA | JAMILA KONDO GEMA | MTAA WA KIPUNGUNI KATA YA KIPAWA | 4/01/2022 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | ZUBERI OMARY KIROBOTO | NYUMBA | MEDADUS LEON SHAO | MTONI MTAA WA BUSTANI | 4/01/2022 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | AMA ABDALLAH KIPENDE | NYUMBA | AMA ABDALLAH KIPENDE | KISARAWE | 18/01/2022 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | MARIANA PATRICK SEDA | NYUMBA | MAILABE MICHAEL BINA | KINYAMWEZI- PUGU | 4/01/2022 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | ALPHANI JAFARI JUMA | NYUMBA | ALPHANI JAFARI JUMA | MIEMBE SABA -KIBAHA | 13/01/2022 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | SHABANI JUMA MAGAZI | NYUMBA | SHABANI JUMA MAGAZI | KILIMA HEWA -KIBAHA | 11/1/2022 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | OMARY SAID MNEMBWE | NYUMBA | OMARY SAID MNEMBWE | MAILI MOJA -KIBAHA | 13/01/2022 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | DOTTO HARUN MSUYA | NYUMBA | DOTTO HARUN MSUYA | TANGINI-KIBAHA | 11/01/2022 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | MAJID ABBAS ZANSE | NYUMBA | MAJID ABBAS ZANSE | VIWEGE - MAJOHE | 28/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | ABDALLAH SEIF MATIMBWA | KIWANJA | ABDALLAH SEIF MATIMBWA | VIWEGE - MAJOHE | 28/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | MDAKI NASSORO KABELELE | NYUMBA | MDAKI NASSORO KABELELE | VIWEGE - MAJOHE | 28/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | LEAH JOHN MPAPALIKA | NYUMBA | LEAH JOHN MPAPALIKA | KIMARA STOP OVER | 27/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | TABU JANETH JULIUS SEDA | NYUMBA | BRAITI SANGA | MAJOHE MJI MPYA | 28/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | GERALD VENANCE SALEHE | NYUMBA | GERALD VENANCE SALEHE | MBEZI MAKABE | 29/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | JAMES PAUL KITONGA | NYUMBA | JAMES PAUL KITONGA | KIVULE | 18/01/2022 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | RANGE DANIEL ROTENTE | 1.KIWANJA 2.NYUMBA | NASHON RANGE ROTENTE NA RANGE DANIEL ROTENTE | PUGU MWAKANGA NA MBONDOLE | 29/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | HUSSEIN LAI SAMIZI | KIWANJA | HUSSEIN LAI SAMIZI | MBONDOLE | 6/01/2022 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | JOHN ELIEZA MUKIZA | NYUMBA | JOHN ELIEZA MUKIZA | KIFURU | 30/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | BOSCO THADEI UTENGA | NYUMBA | BOSCO THADEI UTENGA | KIGEZI JUU | 30/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | WANSAGULA MOSES NATUMWA | NYUMBA | PILI HARUNA BUHANGWA | KINYWAMWEZI-PUGU | 6/01/2022 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | MILLARD MSAMO MUSHI | NYUMBA | MILLARD MSAMO MUSHI | MBEZI MSIGANI | 28/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | GARDNER HATWABY DIBIBI | NYUMBA | ZUWEJA SULEIMAN KAZEMBE | NZASA 'A' | 28/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | PERFECT EMMANUEL GEORGE | NYUMBA | PETER GIBSON MASSAWE | KIMARA BARUTI | 31/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | JULIUS KALANGA LAIZER | NYUMBA | JULIUS KALANGA LAIZER | KATA YA ENGUTOTO –MJI PYA MONDULI | 28/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | HILDA DEOGRATIUS MKAWE | NYUMBA | DEOGRATIAS IGNAS MKAWE | KATA YA DARAJA MBILI MTAA WA NDARVOI | 08/01/2022 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | MAGDALENA KISACK KWAYU | NYUMBA | MAGDALENA KISACK KWAYU | KATA YA LEMARA –ARUSHA | 05/01/2022 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | ARISEN LEONARD SHIRIMA | NYUMBA | ARISEN LEONARD SHIRIMA | KATA YA DARAJA MBILI MTAA WA KATI | 31/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | HULDA FRANK KOMBE | NYUMBA | ESTER POLIKARIPO URIO | KITIENGARE – KIJIJI CHA KIMANDOLU ARUSHA | 11/01/2022 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | EDMUND KAJUNGU MENDRAD | NYUMBA | EDMUND KAJUNGU MENDRAD | KILOLELI - MWANZA | 03/01/2022 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | RWEYEMAMU MENDRAD KABENDERA | NYUMBA | RWEYEMAMU MENDRAD KABENDERA | NYASHISHI MWANZA | 30/12/2021 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | TITO KALAMU SANGA | NYUMBA | TITO KALAMU SANGA | KIBAIGWA | 02/01/2022 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | VICTOR MOSES NKO | NYUMBA | VICTOR MOSES NKO | KIBAIGWA | 02/01/2022 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | HASSAN BAKARI MGAZA | NYUMBA | HASSAN BAKARI MGAZA | HAZINA-DODOMA | 03/01/2022 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | RASHID ATHUMAN MWENDE | NYUMBA | RASHID ATHUMAN MWENDE | MPAMAA-DODOMA | 29/12//2021 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | MOHAMED ATHUMANI BAKARI | NYUMBA | MOHAMED ATHUMANI BAKARI | NDACHI-DODOMA | 28/12/2021 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | KIPEJA TIMBER AND GENERAL SUPPLY | NYUMBA | JOHN TIMOTH PANGANI | IGOMA | 28/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | ELIZABETH JOHN MTUI | NYUMBA | ELIZABETH JOHN MTUI | USA RIVER -NGARESERO | 27/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | MARY BALTAZARY SHAYO | NYUMBA | MARY BALTAZARY SHAYO | SOKONI 1- ENGOSENGIU ARUSHA | 28/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | SIMON BOSCO KOISAN | NYUMBA | SIMON BOSCO KOISAN | ARUMERU-ARUSHA | 29/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | EUNICE ERICAEL SIKAWA | NYUMBA | EUNICE ERICAEL SIKAWA | TENGERU-ARUSHA | 30/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | DICKSON ANICETH GREEN | NYUMBA | DICKSON ANICETH GREEN | LUKOBE BUSWELU-MWANZA | 27/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.NYUMBA (2) 2.KIWANJA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | BUGARIKA IGELEGELE NA BUSWELU MWANZA | 29/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | EDWARD NYAKANYA MSOGOLO | KIWANJA | ROSE ELIAS KISUMO | BUGARIIKA-MWANZA | 31/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | ROBERT THOMAS SERERYA | 1.KIWANJA 2.NYUMBA 3.KIWANJA CHENYE MSINGI | ADELA PETER EZEKIEL | 1.KISHILI NYAMAGANA MWANZA 2.KANGAE"A" NYAKATO MWANZA 3.NSUMBA ILEMELA MWANZA | 30/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | JOHN MISELYA SHIGELA | KIWANJA | JOHN MISELYA SHIGELA | BUJINGWA BUSWELU-MWANZA | 27/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | HASSAN BUGANDA KAPOJONGO | NYUMBA | HASSAN BUGANDA KAPOJONGO | USTAWI-MWANZA | 28/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | ESTER BERNARD KULWIJIRA | NYUMBA | PAUL JULIUS MUHIRI | KIPUNGUNI | 31/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | ASNATI ATHUMAN RAJABU | NYUMBA | ASNATI ATHUMAN RAJABU | SARANGA | 27/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | LEORNARD BAKUZA KABILO | NYUMBA | LEORNARD BAKUZA KABILO | VIWEGE | 29/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | ONESMO PETER MASIMA | NYUMBA | ONESMO PETER MASIMA | MAZIZINI UKONGA | 30/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | SALUM OMARY MTENGWA | NYUMBA | RAMADHANI NASSOR BOMBWE | BUGURUNI | 04/01/2022 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | MASUDI JUMANNE RAMADHANI | NYUMBA | BEATRICE STEPHANO KISHERU | SARANGA KIMARA | 27/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | SHARIFA SAIDI HAMISI | NYUMBA | SHARIFA SAID HAMISI | PUGU BOMBANI | 29/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | JULIUS RYOBA DANIEL | NYUMBA | JULIUS RYOBA DANIEL | KITUNDA | 30/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | VAILETH ERASTO TWEVE | NYUMBA | JOSEPH BENEDICT | KITUNDA KATI | 30/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | NEEMA ARON URIO | NYUMBA | OMARY ATHUMAN MKINDI | KISIWANI SHULE, KIGAMBONI | 05/01/2022 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | GOODLUCK JEROME TARIMO | NYUMBA | JOSEPH REUBEN MATARI | BOKO MAGENGENI | 06/01/2022 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | ATHUMAN HASSAN HEMEDI | NYUMBA | ATHUMAN HASSAN HEMED1 | ULONGONI 'B' | 31/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | MWANAHAMISI KONDO MATAMBO` | NYUMBA | MWANAHAMISI KONDO MATAMBO | RUVU DARAJANI | 07/01/2022 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | AUGUSTINO KILUNDE SANGA | NYUMBA | AUGUSTINO KILUNDE SANGA | TANDALE | 11/01/2022 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | TANDI SAM SIKALANGWE | NYUMBA | TAND SAM SIKALANGWE | PUGU BOMBANI | 29/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | THOMAS REMI MARKUS | NYUMBA | THOMAS REMI MARKUS | TABATA KINYEREZI | 27/12/2021 SAA04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | JUMA NURU MUSHI | NYUMBA | JUMA NURU MUSHI | MBAGALA KUU - TEMEKE | 28/12/2021 SAA 08:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | ABDALLAH SAIDI CHIPALA | NYUMBA | ABDALLAH SAIDI CHIPALA | KITONGOJI CHA MPERA KISEMVULE- MKURANGA | 29/12/2021 SAA04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | BENARD KEMBO NDIEGE | NYUMBA | BENARD KEMBO NDIEGE AND ASHURA SAIDI MCHOPA | KIGAMBONI VIJIBWENI | 28/12/2021 SAA04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | MWETA HAMISI MMBAGA | NYUMBA | MWETA HAMISI MMBAGA | TEGETA 'A' | 10/01/2022 SAA04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KINONDONI | TWAHA RASHID KITATU | NYUMBA | TWAHA RASHID KITATU | MLANDIZI | 4/01/2022 SAA04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | HAMAD ABDALLAH MNEBWE | NYUMBA | HAMAD ABDALLAH MNEBWE | TANDALE SOKONI | 6/01/2022 SAA04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KINONDONI | NGIANA CLEMENCE TEMU | NYUMBA | FATUMA MBARAKA MOHAMED | MBAGALA | 29/12/2021 SAA04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | REHEMA HAMISI JEMEDARI | NYUMBA | REGINA NJENI MWAKESANGULE | MASAKI | 10/01/2022 SAA04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | MUNA SAID NGALENI | NYUMBA | MUNA SAID NASSORO NGALENI | KIGOGO | 6/01/2022 SAA04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | GRACE ELIAS MAHUGI | NYUMBA | GRACE ELIAS MAHUGI AND EMMANUEL KASANZU | MBEZI MALAMBA MAWILI | 4/01/2022 SAA04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | MARIAM PATRICK SHAYO | NYUMBA | DORICE YOHANA MWAKAPESA | MBEZI MSAKUZI | 4/01/2022 SAA04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | ROSE KUNDY JOHN | NYUMBA | ROSE KUNDY JOHN | BAGAMOYO MAPINGA | 3/1/2022 SAA04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | ANGWA CONSTRUCTION COMPANY | NYUMBA | JASSON A. MWAKITWANGE | BUNJU | 5/1/2022 SAA04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | PHIDEA RUTHA BAISI | NYUMBA | PHIDEA RUTHA BAISI | GOBA KINZUDI | 7/1/2022 SAA04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | ANORD CONRAD MTENGA | NYUMBA | ANORD CONRAD MTENGA | SALA SALA | 7/1/2022 SAA04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | IBRAHIM ELIUD MANOSHI | NYUMBA | IBRAHIM ELIUD MANOSHI | VIKAWE KIBAHA | 11/1/2022 SAA04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | SALUM HUSSEN SALUM | NYUMBA | SALUM HUSSEN SALUM | VIKAWE UBAFU | 11/1/2022 SAA04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | RASHIDI SAIDI MSUYA | NYUMBA | RASHIDI SAIDI MSUYA | SAKU MBAGALA | 13/01/2022 SAA04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | ANNA GABRIEL CHUWA | NYUMBA | MUSSA MAGAMBI KASHINDI | CHANIKA NZASA | 13/01/2022 SAA04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | JACOB MWITA MWERA | NYUMBA | JACOB MWITA MWERA | MAPINGA BAGAMOYO | 5/1/2022 SAA04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

| MASHARTI YA MNADA | |
|---|---|
| 1 | Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba au Kiwanja ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14. |
| 2 | Ikiwamnunuziatashindwakutimizashartilolote la mnada kuhusiana na malipo yaawali,hatarudishiwapesayoyotealiyokwishailipa. |
| 3 | Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0714939933/0714467455/0718038313/0768672367/0754497396/0759648448/0752360133/0715363537/0765999000/0713077474/0674821287 |
| 4 | Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote. |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga jipangeni kuwapa mashabiki raha

**USIKU** wa deni haukawii. Hayo ni baadhi ya maneno ambayo huzungumzwa kuhusiana na jambo lililokuwa linasubiriwa kwa hamu na jamii au katika mpira wa miguu, wanaosubiri muda huo huitwa mashabiki.

Leo ni siku nyingine ambayo mashabiki wa soka Tanzania au Afrika Mashariki na Kati watajumuika kufuatilia mechi ya 'dabi' ya Ligi Kuu Bara ambayo inawahusisha Simba na Yanga, zote zina makazi yake Kariakoo jijini Dar es Salaam. Mchezo wa leo ni wa raundi ya nane lakini ni wa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara ambayo inashirikisha klabu 16 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.

Mara ya mwisho timu hizo maarufu kwenye Ukanda huu wa CECAFA zilikutana katika mechi ya Ngao ya Jamii ambayo ni maalumu kwa ajili ya ufunguzi wa msimu huu wa 2021/22, na Simba iliyokuwa chini ya Didier Gomes iliibuka mshindi.

Simba itashuka kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ikiwa na kocha mpya, Mhispania Pablo Franco wakati Yanga yenyewe bado iko na raia wa Tunisia, Nasreddine Nabi, ambaye anaonekana tayari analifahamu 'joto' la dabi hiyo. Kwa sababu mechi hiyo inatarajiwa kufuatiliwa na idadi kubwa ya mashabiki, ni nafasi muhimu kwa wachezaji wa timu hizo kujiandaa kuonyesha soka la kiwango, nidhamu na kujituma kwa faida ya kuondoka na pointi tatu muhimu.

Endapo mchezaji ataonyesha kiwango cha juu katika mechi hiyo muhimu, sio tu ataendelea kuipaisha timu yake, lakini ni sehemu nyingine ya kujitengenezea soko kwa makocha au mawakala wa kimataifa ambao wanasaka vipaji vipya kutoka kwenye bara la Afrika.

Mechi kubwa husaidia kumnyanyua au kumshusha mchezaji, hivyo ni muhimu kila mmoja wao akaliweka hilo kwenye mawazo yake na hatimaye kupitia mechi hiyo ikamsaidia kuanzisha 'mazungumzo' au 'koneksheni' na mawakala wa kimataifa.

Kama ambavyo mshambuliaji wa Tanzania, Simon Msuva aliambiwa na nyota wa Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), anayecheza soka la kulipwa England, hii ni nafasi nyingine kwa nyota wa Simba au Yanga kujitangaza na hatimaye matunda ya kujituma yataonekana. Tunawakumbusha wachezaji wa Simba na Yanga kuhakikisha wanawafurahisha mashabiki wao kwa kuwapa burudani, lakini wafahamu kujituma kwao ndio kutawasaidia kutimiza ndoto zao za kwenda kucheza soka la kulipwa Ulaya kama ilivyo kwa wenzao ambao wameshafanikiwa kufika huko.

Mchezo wa soka ni wa wazi, kama mchezaji utaonyesha kitu cha ziada katika mechi hii, tunaamini mchezo huo uwe 'daraja' la kupata mafanikio kwa kuonekana na vilabu vikubwa na kamwe mawazo yenu yasiishie kucheza soka hapa Afrika Mashariki.

Waamuzi wa mechi hii pia wanatakiwa kufanya kazi yao kwa weledi na umakini wa kiwango cha juu kwa sababu wao ndio wenye nafasi kubwa ya kukamilisha burudani ya mechi hiyo ambayo endapo mmoja wapo ataibuka mshindi, basi atakuwa amepanda hadi kwenye uongozi wa msimamo wa ligi.

Tunawakumbusha waamuzi ambao mmepewa dhamana ya kusimamia mchezo huo kuhakikisha mnazitafsiri vyema sheria 17 za mchezo huo unaopendwa zaidi duniani lakini vile vile mnajiweka kwenye rekodi nzuri ya kuteuliwa kuchezesha mechi nyingine kubwa za kimataifa, hasa zile zinazosimamishwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) na FIFA.

Haipendezi kila baada ya mechi iwe 'dabi' au mchezo mwingine wa ligi unapomalizika, waamuzi wanakuwa ni sehemu ya idara inayolaumiwa kutokana na kuonyesha kiwango cha chini.


Bila kusahau kuwakumbusha mashabiki na wanachama wa timu hizo kuonyesha nidhamu na kujua mipaka yao ya ushangiliaji. Si vyema mashabiki kuonekana wakijichukulia sheria pale watakapoona mambo hayaendi vyema katika upande wao. Wafahamu utovu wa nidhamu unachangia kuharibu 'ladha' ya mechi hii ya watani wa jadi.

Nipashe inawaombea wale wote wanaohusika katika mchezo huu kutekeleza majukumu yao kwa weledi na mafanikio ili timu inayostahili ushindi ipate pointi tatu au kila mmoja apate anachostahili kuvuna.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Afua ni mbili, kufa na kupona

Na Barnabas Maro

**KATIKA** hali mbaya yoyote ile kama ugonjwa, yanayoweza kukutokea ni mawili kuokoka au kufa.

Methali hii hutumiwa kutuhimiza kutojisikitikia kupita kiasi kwa sababu mambo mengi huwa hayamo katika hatua yaani uwezo au mamlaka aliyonayo mtu katika kutengeneza au kufanya jambo.

Kadhalika tunaambiwa: "Ajidhaniaye amesimama aangalie asianguke." Maana yake anayejidhania amesimama anapaswa kuangalia asianguke. Methali hii yatufunza tusiwe na kiburi. Inawakanya wenye vyeo wajichunge kwa kuwa wanaweza kuharibikiwa na kuwa si chochote.

Bado naendelea kuzishauri Simba na Yanga kuwa: "Ukijidhani umesimama unapaswa kuangalia usianguke."

Methali hii hutumiwa kwa mtu anayejitapa kutokana na hali nzuri aliyonayo, mathalan ya kiuchumi. Anapaswa kukumbuka hali hiyo inaweza kumwondokea na akabaki kama mwanzoni.

Timu za Simba na Yanga zinazoitwa eti 'watani wa jadi' mimi huwaita 'wachukianao wawili' kwani hakuna wanachama wala mashabiki, yaani watu wenye mapenzi na hamasa kubwa juu ya jambo au kitu fulani, wanaopenda mojawapo ya timu hizo, wanaotaka au kufurahia ushindi wa upande mwingine.

Kwa hiyo ni dhahiri walivyosema wahenga kuwa: "Uchongwao huchongewa paa ulimwengu ukamsawaa." Maana yake mti uliochongwa kwa nia ya kutumiwa katika paa huweza kuishia kumchoma au kumfuma binadamu.

Methali hii huweza kutumiwa kwa mtu aliyefanya ubaya fulani akiudhamiria mtu mwingine kisha ukamrudia yeye mwenyewe. Twanasihiwa tusiwatendee wenzetu mambo mabaya kwani ubaya hatima yake mbaya.

"Uchungu mwenenda nao, shingo ujeze matama." Maana yake uchungu alionao mtu unaijaza shingo yake sumu. Huweza kutumiwa kwa mtu anayeweka kinyongo au uchungu wa ndani kisha aipatapo nafasi akaishia kuyasema mabaya, hasa kumhusu aliyemkasirikia.

Ghiliba ni udanganyifu wenye nia ya kujinufaisha ilhali ghilibu ni kitendo cha kudanganya kwa madhumuni ya kujinufaisha tu. Kwanini Simba na Yanga zachukiana kama Wayahudi na Waarabu?

Nimeeleza mara nyingi kuwa "chuki humchoma anayeihifadhi kwani humsumbua anayeiweka chuki hiyo. Kuhusu chuki, nimeeleza mara kadhaa na kuwataja Simba na Yanga lakini ni kama nimewachochea!

"Mchezo" ni jambo linalofanywa kwa nia ya kuburudisha. Jambo ambalo watu au timu hulifanya kwa kushindana ili kupata mshindi, jambo ambalo mtu hufanya kwa kupitisha wakati au kujifurahisha. Ghiliba na chuki kati ya Simba na Yanga zatokea wapi kama sio upumbavu na chuki zisizo na maana?

"Ebo!" Hawa mafahali wawili wa Tanzania Bara wanapaswa kuacha ubozi (upumbavu, ujuha, ujinga) wao na wajue kuwa fahali wawili hawawezi kukaa zizi moja kwa kuwa kila mmoja anataka awe mkuu wa zizi kwahiyo watashinda wakipigana kutwa!

Simba na Yanga zinapaswa kusoma na kutafakari (kitendo cha kuzingatia jambo kwa makini) methali hii: "Atupaye tope hujichafua naye." Yaani mtu anayetupa au anayerusha tope huishia kujichafua.

Kwa ufupi, anaye jihusisha na ubaya au mabaya huishia kujiharibia sifa zake. Huweza kutumiwa kwa mtu anayesema mabaya kuwahusu watu wengine na yakamrudia!

Leo tunataka kuona mchezo mzuri usio na ghadhabu, chuki wala vurugu. Kadhalika marefarii wafanye maamuzi sahihi na ya haki bila upendeleo wa aina yoyote.

Wachezaji waungwana hupeana mikono baada ya mechi kwa walioshindwa kuwashika mikono walioshinda sio kuwakimbia au kutukanana. Huo ndiyo uungwana.

marobarnabas@yahoo.com 0784 334 096

# Taasisi yataka mafanikio ya Uhuru yalindwe

**Na Sabato Kasika**

WATANZANIA wametakiwa kulinda mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru ikiwamo umoja wa kitaifa na mshikamano wao kwa ajili ya manufaa yao na ya vizazi vijavyo.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya jijini Dar es Salaam, wakati akitoa salamu za taasisi za miaka 60 ya uhuru.

Ngawaiya alisema tangu mwaka 1961 wakati nchi inapata uhuru hadi sasa, kuna mafanikio katika nyanja mbalimbali ambayo nchi imeyapata, ambayo yanatokana na kupambana na maadui ujinga, maradhi na umaskini.

"Miaka 10 ya kwanza chini ya uongozi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, uchumi ulikua kwa kasi huku huduma za kijamii nazo zikiimarika, baadhi ya huduma hizo ni elimu, afya na nyingine nyingi," alisema Ngawaiya.

Alisema elimu ilitolewa bure kuanzia msingi hadi chuo kikuu, matibabu yalikuwa bure katika hospitali zote za serikali, na kwamba wakoloni waliitwa kuja kuona jinsi ambavyo nchi ilikuwa ikichanja mbunga kwenda mbele.

Alifafanua kuwa katika kipindi hicho, nchi iliimarisha umoja na mshikamano wa kitaifa kwa kuondoa ukabila na udini na kwamba hadi sasa hayo yaliendelezwa na awamu zilizofuata na hata iliopo sasa.

"Serikali ilitaifisha mashamba, ardhi, viwanda na nyumba na kuvifanya kuwa mali ya umma, ujamaa na kujitegemea ulianzishwa na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kipekee kung'ara barani Afrika," alisema.

Alisema, ndani ya miaka 60 ya uhuru, mafanikio ni mengi kuanzia, kisiasa, kijamii na kiuchumi, huku akiwataka Watanzania kuyalinda kwa ajili yao na hata kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

Mwenyekiti huyo alisema, miaka saba ya mwisho ya serikali ya awamu ya kwanza, ilikumbana na hali mbaya ya uchumi, lakini awamu ya pili ikavikabili na kuifanya Tanzania kuendelea kuwa imara.

Kiongozi huyo alisema, awamu zilizofuata hadi ya sita iliyopo sasa, zimeendelea kusimamia mafanikio ambayo Tanzania imeyapata hasa kwa kupigana na maadui watatu ambao ni ujinga, maraddhi na umaskini.

"Jambo lingine la kujivunia ni utaratibu wa kupokezana kijiti cha uongozi kwa amani, ingawa kumekuwapo na changamoto za hapa na pale kwenye uchaguzi mkuu ambazo husababisha malalamiko kutoka vyama vya upinzani," alisema.

Aidha, alisema CEGODETA inatoa wito kwa serikali ya awamu ya sita kuendeleza mazuri ya awamu zote na kuwataka wananchi kusaidia kwa vitendo kuendeleza tunu za taifa ambazo ni amani, umoja na mshikamano.

Kiongozi huyo anafafanua kuwa serikali hiyo inaendeleza miradi yote iliyoachwa na awamu ya tano na pia inaboresha utawala bora kwa kuondoa mahakamani kesi za muda mrefu bila kusikilizwa kwa kukosekana ushahidi.

Alisema, CEGODETA inatoa wito kwa serikali ya awamu ya sita kuendeleza mazuri ya awamu zote na pia inawataka wananchi kusaidia kwa vitendo kuendeleza tunu za taifa ambazo ni amani, umoja na mshikamano.

# Waziri asema ukiukwaji haki za binadamu bado ni tatizo

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema pamoja na kuwapo sheria kali za kudhibiti makosa ya jinai, bado kuna ukiukwaji wa haki za binadamu ikiwamo mauaji, ubakaji na ulawiti kwa watoto.

Hali hiyo inatokana na ongezeko la matukio ya vitendo hivyo ambapo kuanzia Januari hadi sasa yamefikia 6,168.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam kwenye maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Haki za Binadamu, inayoadhimishwa kila mwaka Desemba 10 duniani.

Alisema haki iliyo kuu na ya msingi ni ya kuishi, ingawa bado yako matukio ya mauaji yatokanayo na wivu wa kimapenzi na imani potofu za kishirikina, ambayo hukatiza uhai wa watu.

"Ukatili dhidi ya wanawake bado ni tatizo. Kuanzia Januari mwaka huu kati ya matukio 6,168 watoto ndiyo waathirika wakubwa.

Watoto waliobakwa ni 3,524 na waliolawitiwa 637, waliochomwa moto 130 na waliopata mimba ni 1,877 katika hili watuhumiwa ni 3,800.

"Wakati tukiadhimisha miaka 60 ya Uhuru, uwe ni uhuru wa watu, haki na usawa. Nikiwa Waziri na msimamizi wa vyombo vyenye maudhui ya haki za binadamu, nitaendelea kulinda na kuiheshimu haki hii," alisema Simbachawene.

Alisema Sheria ya Adhabu Na. 20 pamoja na marekebisho yake mwaka 2019, dhidi ya vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu, inaeleza namna ya kuwashughulikia wahalifu na uendeshaji kesi, bado matukio yanatokea ndani ya jamii.

"Wizara kwa kushirikiana na ofisi ya DPP (Mkurugenzi wa Mashtaka), tuna kikosi kazi ambacho kinafanya kazi ya kupitia Magereza kuangalia na kuhakikisha kesi za muda mrefu bila ushahidi zinafutwa," alisema Simbachawene.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema tamko la dunia la haki za binadamu, lililoidhinishwa na Umoja wa Mataifa mwaka 1948, lenye ibara 30, linaelezea misingi ya haki.

"Ibara ya 3 inasema kila mtu ana haki ya kuishi, haki ya uhuru na haki ya kulinda nafsi yake, na Ibara ya 26 inasema kila mtu ana haki ya kupata elimu. Elimu yapasa itolewe bure hasa ya msingi," alisema Henga.

Balozi wa Norway nchini, Elizabeth Jacobson, alisema hatua ya serikali ya Tanzania kuwarejesha masomoni wasichana waliopata mimba shuleni ni kati ya haki za msingi za binadamu na kutomwacha nyuma mwanamke katika maendeleo.

"Tanzania katika miaka 60 ya uhuru, pia uwepo uhuru wa kujieleza, demokrasia kwa sababu vina uhusiano katika suala la haki za binadamu," alisema Balozi.

Mratibu Mkazi wa kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa (UN), Zlatan Milisic, alisema wakati dunia inakumbwa na changamoto za corona na mabadiliko ya tabianchi, yako makundi ambayo huachwa nyuma, wakiwamo watu wenye ulemavu na wanawake, watoto, licha ya nchi wanachama kuahidi kulinda haki za binadamu.



Ofisa Masoko wa Wilaya ya Temeke, mkoani Dar es Salaam, Doto Killangi akizungumza katika uzinduzi wa kampeni ya 'Safari Salama kwa Wasichana na Wanafunzi Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana' wilayani humo juzi, iliyoandaliwa na shirika la wanawake katika jitihada za kimaendeleo (WAJIKI). Kulia ni Mwenyekiti wa Bodi wa shirika hilo, Kalunde Mongomongo na Mkurugenzi wake, Jathen Mawinza. **MPICHA: SABATO KASIKA**

# REPOA yataka habari zilizosheheni takwimu

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti na Kupunguza Umaskini (REPOA), Dk. Donald Mmari, amewataka waandishi wa habari kutumia taarifa za kitafiti katika uandishi wao, ili Watanzania wafikiwe na habari zilizochakatwa.

Katika ufunguzi wa mafunzo kwa waandishi wa habari mkoani Dar es Saalam jana, Dk. Mmari alitoa rai hiyo kwa kada hiyo muhimu.

Alisema REPOA inatambua wajibu wa waandishi wa habari katika kuelimisha umma na kuwakumbusha kuwa wana nguvu ya kuandika kitu kikagawa au kuunganisha jamii.

"Tunavitegemea vyombo vya habari kubadilisha fikra za Watanzania. Ni muhimu waandishi wa habari mkatumia taarifa za kitafiti ili wananchi wafikiwe na habari zilizochakatwa vizuri," alikumbusha.

Dk. Mmari alitoa mfano mauaji ya kimbari yaliyotokea mwaka 1994 huko Rwanda na kubainisha kuwa vyombo vya habari vilichangia kuchochea mauaji hayo.

"Mnachokiandika kinaweza kuingia kwenye vichwa vya Watanzania na wakaamini na wakawaamini sana. Kwa hiyo, muwe makini katika kuandika habari zetu.

"Ni vizuri unapoandika habari ya mradi fulani uliofeli, ujue chimbuko lake, kwa nini haujakidhi matakwa? Mnaweza kujikita na taasisi zinazofanya utafiti ili mnapohabarisha umma mradi huu umefeli na sababu zake ni hizi na mapendekezo ya kulingana na utafiti ni haya," alisema.

Kuhusu mafunzo hayo, Dk. Mmari alisema lengo lake ni kuangalia kama watafiti wanaona namna wanavyoweza kuwafikia wananchi.

Alisema mafunzo kama hayo yamekuwa yakitolewa kwa wabunge, watumishi wa serikali na idara mbalimbali na kusisitiza kuwa wataendelea kuyatoa.

# Uboreshaji sera kunufaisha wakulima mpunga

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SHIRIKA la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) kwa kushirikiana na serikali pamoja na wadau mbalimbali wa mpunga, limeanza kuzipitia sera zilizopo na kuziboresha ili kuwasaidia wakulima wa zao hilo kupata masoko ndani na nje ya nchi.

Katika kufikia malengo hayo, FAO kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) na Shirika la Kimataifa la Utafiti wa Mpunga (IRRI), limeanza mapitio ya sera kwa ajili ya kumsaidia mzalishaji wa mpunga kupata pembejeo za uhakika kama mbegu na mbolea wakati wa kilimo.

Akizungumza katika mkutano wa wadau hao, Mratibu wa Mradi wa Kujenga Uwezo na Kubadilishana Uzoefu katika zao la mpunga kutoka FAO, Diomedes Kalisa, alisema kwa sasa uzalishaji wa mpunga nchini umeongezeka lakini bado kuna tatizo upande wa sera. Kalisa alisema lengo kubwa la mkutano huo ni kuangalia kwa pamoja upande wa sera, kutokana na Tanzania kwa sasa kujitosheleza kwa mpunga na kuongeza uzalishaji ambao unahitaji masoko ya nje na ndani.

"Kwa sasa Tanzania tunajitosheleza kwenye mpunga, lakini tukiangalia utoshelezaji unajitokeza pale tunapoongeza maeneo ya kilimo tunapoendelea kuongeza uzalishaji, mchele wetu unaenda wapi?" alihoji.

Kwa mujibu wa mratibu huyo, mkakati uliopo kwa sasa baada ya kujitosheleza ni kuweka mipango ya kusafirisha mchele nje ya nchi, hivyo ni lazima kuweka sera rafiki ya kufanikisha hayo.

"Tunaangalia kwenye sera zetu kama tuna mambo rafiki ambayo yanawezesha kuhakikisha hayo tunayafikia, kupata masoko yanayojitosheleza au tunayo mipango rafiki inayoangalia kwa upande wa pembejeo, mbolea, mbegu na je kuna vitu vyovyote ambavyo tunaweza kufanya maboresho?" alisema Kalisa.

Mkulima wa mpunga tarafa ya Pawaga mkoani Iringa, Twalibu Ubwa, alisema mbali na mafanikio waliyoyapata ikiwamo kuongeza uzalishaji wa zao hilo la mpunga, bado wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo uhaba wa masoko hali inayosababisha mchele kuwa na thamani ya chini.

Alitaja changamoto nyingine kuwa ni kukosekana kwa elimu ya kutosha katika kilimo cha zao hilo ili kuongeza uzalishaji kwa kulima eneo dogo na kupata mavuno mengi kama nchi zingine hatua ambayo itasaidia pia kukuza uchumi wa wakulima.

Meneja wa TARI Kituo cha Utafiti wa Mpunga, Ifakara mkoani Morogoro, Dk. Atugonza Bilaro, alisema wameanza kuzalisha mbegu zinazoleta tija kwa mkulima kulima eneo dogo na wako baadhi ya wakulima wameanza kunufaika kupitia mbegu hizo.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Uthibiti wa Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) Patrick Ngwediagi, alisema serikali inawaunga mkono wadau na kwamba itafanyia kazi kile watakachokipendekeza katika mchakato unaoendelea wa kuboresha Sera ya Kilimo ya mwaka 2013.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Afrika Tanzania, Adam Mihayo (katikati), akiwa na watendaji wakuu wa kampuni za bima za Alliance General, Rajiv Kumar (kushoto), K.V.A Krisha (wa pili kushoto), Mtendaji Mkuu wa Alliance Life, Byford Mutimusakwa (wa pili kulia) na Mkuu wa Kitengo cha Bima wa benki hiyo, Eva Kakwale, wakati wa uzinduzi wa huduma ya Bima Kwanza ya benki hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## TFS yatakiwa kuanzisha vikundi kutunza mazingira

**Na Julieth Mkireri,**
MKURANGA

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Mashariki, imetakiwa kutembelea shule na kuunda vikundi vya wanafunzi vya kutunza mazingira ambavyo vitatumika katika kueneza elimu kwenye maeneo mbalimbali.

Wito huo ulitolewa jana katika msitu wa Vikindu kwenye maadhimisho ya Uhuru na mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya wilaya ya Mkuranga, Salum Mwamfula, yaliyoandaliwa na TFS Kanda ya Mashariki.

Alisema vikundi hivyo vitasaidia kutoa elimu kwenye jamii na kutumia kutunza mazingira na misitu iliyo karibu kwenye jamii inayowazunguka ikiwamo shule wanazosoma.

Kamanda wa TFS Kanda ya Mashariki, Kamishna Msaidizi Caroline Mallundo, alisema utalii ni chanzo cha kukuza uchumi nchini ambacho pia kinatumika kuinua kipato cha wananchi.

Mallundo aliwataka wananchi kutunza misitu iliyopo karibu na maeneo yao ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mhifadhi wa Wilaya ya Mkuranga, Charles Kaselya, alisema hifadhi ya msitu wa Vikindu ilianza mwaka 1947 na kwamba ina aina 65 za miti, bwawa la asili na daraja la asili la mbao ambalo ni kivutio cha utalii.

Alisema vikwazo wanavyokumbana navyo ni pamoja na uvunaji haramu wa mazao ya misitu kutokana msitu huo kuwa karibu na mji.

Kikwazo kingine, alikitaja kuwa ni uingiaji wa mifugo katika msitu huo na ubovu wa miundombinu ya kuingia katika msitu huo.

# Vifo vya uzazi vyazidi kupungua Shinyanga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

VIFO vya mama na mtoto vitokanavyo na uzazi mkoani Shinyanga, vimeendelea kupungua kutokana na utolewaji wa elimu ya afya ya uzazi, na uboreshaji wa huduma za afya kuwa karibu na wananchi.

Mratibu Huduma Afya ya Uzazi na Mtoto mkoani Shinyanga, Joyce Kondoro, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa.

Alisema ndani ya miaka mitatu, mkoa umepunguza kwa kiasi kikubwa vifo vya mama na mtoto vitokanavyo na uzazi, tofauti na miaka ya nyuma ambapo hali ilikuwa mbaya.

"Takwimu za vifo vya uzazi kwa kinamama mwaka 2019 zilikuwa vifo 50, mwaka 2020 vifo 46 na mwaka huu tuna takwimu hadi za Juni ambazo zinaonyesha vifo vya kinamama kutokana na uzazi ni 15," alisema.

"Vifo vya watoto wachanga mwaka 2019 vilikuwa 866, mwaka jana 567 na mwaka huu hadi Juni tuna vifo 270 na tutaendelea kupunguza zaidi vifo hivi vitokanavyo na uzazi kwa nguvu zote," aliongeza.

Kondoro alisema katika kupunguza vifo hivyo, mkoa umevipandisha hadhi vituo vya afya 18 kuanza kutoa huduma ya dharura ya afya ya uzazi kwa mama na mtoto na kupunguza umbali wa huduma hiyo kwa wajawazito.

Pia alisema wamekuwa wakiendelea na utoaji wa elimu ya afya ya uzazi kwa kinamama pamoja na kuzingatia uzazi wa mpango ili kuacha kuzaa mfululizo jambo ambalo limekuwa likichangia vifo vingi vya uzazi.

Alisema wamekuwa wakitoa na elimu ya kujitambua kwa wasichana wadogo hospitalini hapo katika chumba maalumu ikiwamo masuala ya afya ya uzazi, kujitambua na kuacha ngono katika umri mdogo na kwa wale ambao wana ujauzito wanawapatia huduma stahiki na kwa ukaribu ili kuokoa maisha yao na mtoto.

Nao baadhi ya kinamama mkoani Shinyanga, waliipongeza serikali kwa kuendelea kuboresha huduma za afya ambazo zimekuwa na mchango mkubwa wa kuhamasisha wanawake kuacha kujifungulia nyumbani na kwenda hospitalini maeneo ambayo ni salama kwao.



# Wizara yatia saini kuongeza ufanisi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Maji imetia saini mkataba wa ufanisi na utendaji kazi wa mabonde ya maji tisa kwa lengo la kuangalia uboreshaji unaofanywa na bodi hizo hapa nchini kila mwaka.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga, alisema utiaji saini huo hufanyika kila mwaka kwa lengo la kuhakikisha mabonde hayo yanafanya kazi kwa ufanisi ili Watanzania wapate maji kwa wakati na kuepuka mgawo.

Alisema kutokana na utiaji saini wanaofanya mwaka huu, ufanisi umepanda kutoka asilimia 52.9 hadi asilimia 75.2 kwa mwaka 2021.

Katibu Mkuu Sanga alisema pamoja na ufanisi huo kupanda, wanatakiwa kwenda kuongeza bidii katika utendaji kazi ili kuhakikisha wanafikia asilimia 100 jambo ambalo litachangia watu kupata maji kwa wingi.

Alisema pamoja na kuwa na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi, bodi hizo zinapaswa kukabiliana nayo kwa sababu changamoto hiyo iko duniani kote na si Tanzania pekee.

Sanga alisema kina cha maji hutegemea mvua zaidi lakini mvua zinapochelewa inabidi kuwe na namna ya kuhakikisha maji yanapatikana kwa sababu wizara ya maji ndio waangaalizi wa sekta hiyo.

Alisema mvua zilizoanza kunyesha ziwe fursa katika mabonde hayo kuhakikisha maji hayo yanatumika katika kuboresha upatikanaji wa maji hapa nchini katika maeneo mbalimbali.

Kwa mujibu wa Sanga, wanapaswa kujenga mabwawa kwa ajili ya kuzuia maji ya mvua yasiende baharini badala yake yatumike kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa maji.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mhandisi Nadhifa Kemikimba, aliwataka wahandisi wa mabonde hayo kwenda kutekeleza maagizo waliyopewa ili kuweka sekta hiyo imara katika utoaji huduma ya maji.

Alisema kitendo cha Waziri Mkuu kwenda kutembelea katika baadhi ya vyanzo vya maji si jambo jema inaonyesha jinsi gani wao wamelala katika utendaji wao.

# Katibu awataka wanasiasa kuhamasisha chanjo corona

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KATIBU MKUU wa Chama cha Wakulima (AAFP), Rashid Rai, amewataka viongozi wa siasa kuunga mkono juhudi za serikali kuwahamasisha Watanzania kujitokeza kwa hiari kuchanja chanjo ya corona.

Rai alitoa rai hiyo juzi wakati wa uzinduzi wa mpango mkakati wa kuhamasisha wananchi kuchanja chanjo ya ugonjwa huo, uliofanyika katika ofisi za chama hicho Chadulu, jijini hapa.

Alisema viongozi wa vyama vya siasa wanayo nafasi kubwa ya kuhamasisha watu wao kushiriki suala hilo ambalo serikali imegharimia mamilioni ya fedha kwa ajili ya kuwawezesha Watanzania kuchanja kwa hiari na bure.

"Viongozi wa siasa bado jambo hili hawajaitikia vya kutosha, hivyo nitoe wito kwa taasisi mbalimbali Watanzania kujitokeza kuchanja ili kumuunga mkono Rais wetu ambaye ameonyesha mfano wa kuchanja," alisema Rai.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameonyesha njia ya kuwaongoza Watanzani, hivyo viongozi wa serikali washiriki kikamilifu kuwahamasisha watu wachanje chanjo hiyo ili kujilinda na janga la corona.

Naye muuguzi wa Kituo cha Afya Makole, Shecky Cobb, aliviomba vyombo vya habari kuwaelimisha Watanzania ili kufikiwa kupata huduma hiyo ambayo inatolewa bure.

Kadhalika, alisema serikali na viongozi wa siasa pekee yake hawawezi kuwafikia kuwashawishi Watanzania hao ili kushiriki kuchanja ila kwa kutumia vyombo vya habari wanaweza kufanikisha jambo hilo.

Mwenyekiti wa vijana wa chama cha hicho, Mark Mhemela, aliwahamasisha vijana kuwa mstari wa mbele kujitokeza ili kushiriki zoezi hilo muhimu kwa maendeleo ya afya zao.

Pia aliwataka vijana kuondokana na propaganda na taarifa zinazotolewa zisizo za kweli ambazo zinazopotosha kuhusu kirusi kilichoibuka badala yake wajitokeze kwa wingi kuchanja.

Hata hivyo, alisema kirusi kilichoibuka hivi karibuni hakichagui kama kilichokuwa kimejitokeza mwanzo, hivyo vijana wanatakiwa kumuunga mkono Rais ikizingatiwa kuwa wao ndio nguvu kazi ya taifa.



Muuguzi wa kituo cha afya cha Makole, Shecky Cobb (kulia), akitoa elimu ya umuhimu wa kuchanja chanjo ya Uviko-19, katika kikao cha uhamasishaji kwa viongozi wa chama cha Alliance for African Farmers Party (AAFP), katika kata ya Makole, kitongoji cha Chadulu, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Waitara ataka ukaguzi viwanja vya ndege

**Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, ameiagiza Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) kufanya ukaguzi wa kina katika viwanja vya ndege nchini, huku akisisitiza kila mtu lazima akaguliwe ili kuepuka kirusi kipya cha ugonjwa wa corona ili kisiingie nchini.

Waitara aliyasema hayo juzi katika mkutano wa taasisi pamoja na wafanyakazi wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi uliofanyika jijini hapa.

Alisema Rais Samia anahangaika kutangaza utalii lakini TCAA haishughuliki kukagua watalii jambo linaloweza kuchangia kupunguza idadi yao kwa kuhofia mlipuko wa wimbi la nne la virusi vya corona.

"Naomba fanyeni ukaguzi kwa kila mtu na si kusema huyu ni mwanadiplomasia jambo ambalo halikubaliki katika afya," alisema Waitara.

Pia alimuagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo na Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA) kuhakikisha wanashughulikia suala la mzabuni anayetengeneza mfumo wa kudhibiti mwendo na kama anastahili kuendelea kuwapo kutokana na kulalamikiwa na wasafirishaji.

Kadhalika alizitaka Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) kuacha kuchelewesha miradi ya serikali wanayopewa kutekelezwa ili kuepuka kupoteza wateja.

Alisema ni jambo la kushangaza mzabuni aliyeshinda tenda ya mara ya kwanza ya Sh. billion 1.2, amepokonywa na kutangazwa nyingine ambapo aliyepata analalamikiwa na wasafirishaji kutokana na kutoa takwimu za uongo.

Waitara alisema kumekuwa na malalamiko kutoka kwa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA) kutokana na mzabuni huyo kushindwa kudhibiti mwendo hadi apige simu makao makuu ili kujua dereva anakwenda mwendo gani.

"Unakuta mtu anakwenda 'speed' mwendokasi 80 lakini zaidi ya hapo mashine zinashindwa kujua gari linakwenda 'speed' ngapi," alisema Waitara.

Alisema tatizo hilo limekuwa la muda mrefu hivyo katibu na mtendaji mkuu wa LATRA anapaswa kulishughulikia ili wasafirishaji kuwa salama.

Kuhusu TEMESA, alisema wafanyakazi wake wamekuwa hawatengenezi magari kwa wakati, huku akiwaonya Tanroad kutangaza tenda za kishikaji na kupeana wao wenyewe tenda hizo.

Alisema watendaji wa TEMESA wanawachukua mafundi wa taasisi hiyo na kuwapeleka katika gereji zao jambo ambalo inachangia kupoteza wateja.

Kwa upande wa TBA alisema imekuwa ikichelewesha miradi mingi ya ujenzi ya serikali bila kujua tatizo ni lipi kwani hali hiyo inachangia kupoteza wateja pamoja na imani ya kukabidhiwa kazi.





# Shirika lasisitiza uhuru wa vyombo vya habari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUFUNZI Mwandamizi kutoka Shirika la Internews Tanzania, Alakok Mayombo, amesema uhuru wa vyombo vya habari ni suala muhimu kwa kuwa linahusiana na haki za binadamu.

Mayombo aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo kwa waandishi wa habari kuhusu haki za binadamu yaliyofanyika kwa njia ya mtandao (zoom). Mafunzo hayo yaliandaliwa na Internews.

Alisema endapo jamii itapata habari kwa wakati, huwa na nafasi nzuri ya kufanya uamuzi sahihi katika masuala mbalimbali yakiwamo ya kiafya, kiuchumi na kijamii.

Kwa mujibu wa Mayombo, vyombo vya habari vina mchango mkubwa katika maendeleo ya jamii, hivyo ili uhuru wa vyombo hivyo upatikane na kufanya kazi vizuri, suala la sera na sheria halina budi kuzingatiwa.

Alisema vyombo vya habari vinakuza demokrasia, utawala bora na haki za binadamu vinapofanya kazi vizuri, hivyo kusaidia jamii kupata haki.

Pia alisema ili vyombo vya habari vitumike kuchangia maendeleo ya nchi, kunahitajika uhuru wa haki za binadamu.

Naye Patrick Kipangula kutoka Idara ya Habari (MAELEZO), aliwataka waandishi wa habari wazisome sheria za habari ili kuzifahamu na kwamba kutoa habari kwa jamii ni takwa la kisheria.

Aliwataka waandishi wa habari wafanye kazi zao za kutoa taarifa kwa jamii kwa weledi kwa sababu wanalindwa na Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977.

Akitoa mada katika mafunzo hayo, mwandishi mwandamizi wa Zanzibar, Aima Duwe, alisema Sheria ya Zanzibar kifungu 24 kimeeleza kuwa watu wote watakuwa na uhuru kwenye misingi ya haki za binadamu bila ya kuathiriwa kwa manufaa ya umma.

Baadhi ya washiriki wa mkutano huo walisema uwapo wa sheria za habari zinawafaidisha wananchi wote na si waandishi wa habari pekee kwa sababu wananchi ndio walengwa katika kupata taarifa.

"Kuna haja ya kupigiwa debe katika kukuza tasnia ya habari na kufanya uhuru wa habari kuwa mzuri kwa manufaa ya wananchi," alisema Ali Mbarouk mwandishi wa habari kutoka kisiwani Pemba.



Mtafiti kutoka Taasisi ya utafiti ya World Vegetable Center ya Arusha, Jeremiah Sigalla (kulia), akiangalia bidhaa ya mafuta ya karafuu kutoka kwa mmoja wa wajasiriamali katika maonyesho ya bidhaa za viungo katika Hoteli ya Mesasi, Kisiwani Pemba juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# 'Hamasisheni wanawake kudai haki za uongozi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa Ali, amewataka wahamasishaji jamii kuhamasisha wanawake kudai haki zao za uongozi na demokrasia kisiwani Pemba.

Pia amesema wanapaswa kuendelea kufuatilia na kuibua changamoto zinazowakwaza wanawake kukosa haki zao katika nyanja mbalimbali kwenye jamii.

Dk. Mzuri aliyasema hayo jana wakati wa mkutano kati ya watendaji wa TAMWA na wahamasishaji wa kutetea haki za wanawake, wenye lengo la kujadili na kutathmini maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa uongozi na demokrasia kwa wanawake uliofanyika kisiwani humo na kufadhiliwa na Ubalozi wa Norway.

Alisema lengo la mradi kuwatumia wahamasishaji hao ni kutaka wafanye kazi ya kukutana na wanajamii kwa lengo la kubaini changamoto zinazowakabili na kuwajengea uwezo wa kudai haki zao katika masuala mbalimbali ikiwamo demokrasia na uongozi.

"Jukumu letu ni kumulika uwajibikaji wa kila mmoja au taasisi ili kufuatilia uwazi, uwajibikaji na upatikanaji wa haki za wanawake kwenye jamii katika kila nyanja,"alisema.

Pia alisisitiza ufuatiliaji wa karibu wa changamoto zote zinazoibuliwa katika jamii ili kutatuliwa na ngazi husika kwa wakati kutokana na mradi huo kutojikita katika masuala ya uongozi pekee.

"Kuendelea kufanya mikutano na wanajamii na kuibua changamoto nyingi pasipo kuzitafutia ufumbuzi wa suluhu yake itakuwa hatujafanya kitu na lengo la wahamasishaji jamii katika mradi huu ni kuhakikisha tunaibua changamoto na kuzifanyia ufuatiliaji wa karibu ili wanawake wapate haki zao zote," alisema Dk. Mzuri.

Alitaja miongoni mwa maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa ufuatiliaji wa karibu na wahamasishaji hao kuwa ni pamoja na upatikanaji wa huduma za afya, wanawake kukosa vitambulisho vya mzanzibari mkaazi na uhaba wa huduma za kijamii.

Naye Mkurugenzi wa Pemba Envromental, Gerder and Advocacy (PEGAO), Hafidh Abdi Said, alisema wahamasishaji hao wamefanya kazi kubwa ya kuifikia jamii na kufanikiwa kuibua changamoto mbalimbali ambazo zinaendelea kufanyiwa kazi.

"Baada ya kufanya kazi kubwa ya kuifikia jamii kuihamasisha imeonekana zipo changamoto nyingi zilizoibuliwa na zinahitaji kufanyiwa kazi ili malengo ya mradi wetu yakamilike," alisema Hafidh.

Rukia Ibrahim, mmoja wa wahamasishaji hao kutoka Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba alisema hamu yao ni kuifikia wilaya yote na kuzibaini changamoto zinazowakabili wanawake na kuzifanyia utetezi kwenye ngazi husika.

"Kwa mfano kwenye mikutano yetu tulibaini uwepo wa huduma dhaifu kwenye vituo vya afya mbalimbali katika Wilaya ya Wete, baada ya kulibaini hilo tutalifikisha kwa wahusika na hatua zaidi zinaendelea kuchukuliwa,'' alisema.

# DC awataka vijana kuchangamkia fursa katika sekta ya mawasiliano

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Wilaya ya Magharibi A Unguja, Suzan Peter Kunambi, amewataka vijana kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kuchangamkia fursa zilizopo katika sekta ya mawasiliano.

Akizungumza jana katika sherehe ya kuwatunuku vyeti wahitimu wa mafunzo ya TEHAMA kwa vijana, yaliyofanyika katika Kituo cha Elimu na Ubunifu wa Kisayansi, Mwera Regeza Mwendo wilayani humo, alisema mafunzo waliyoyapata yawe chachu ya kutumia vizuri TEHAMA kwa kujipatia fursa za ajira ,masoko ya bidhaa, taaluma zaidi na ubunifu.

Kunambi alisema umefika wakati kwa vijana kuwa na matumizi sahihi ya teknolojia ili yawaletee faida wao binafsi, taifa na jamii kwa ujumla.

Aliwataka vijana kuyatumia vizuri mafunzo hayo na kuyafanyia kazi kwa vitendo kwa lengo la kujitengenezea mazingira ya kujiajiri au kuajiriwa katika eneo hilo la TEHAMA.

Mkuu huyo aliwapongeza wahitimu wa mafunzo hayo kwa uamuzi wao katika kushiriki pragramu na kutoa wito kwa wengine kuiga mfano wa walimu hao ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya matumizi ya teknolojia duniani.

Alisema lengo la serikali ya Zanzibar kujenga vituo hivyo vya elimu ya ubunifu wa kisayansi ni kuona walimu, wanafunzi na jamii wananufaika kwa kuongeza uwezo utakaosaidia kukuza maendeleo ya nchi.

Akisoma risala kwa niaba ya wahitimu wenzake, Abdul-razak Khamiss Sheha alisema moja ya changamoto katika kituo hicho ni kukosa kiyoyozi katika chumba cha darasa la kompyuta kutokana na joto lililomo ndani ya chumba hicho.

Naye Kaimu Mratibu wa HAB, Maulidi Suleiman Ali, alisema kituo hicho kimejipanga kuanzisha programu maalumu kwa walimu wa msingi wanaofundisha masomo ya Sayansi, Hisabati na Kiingereza katika wilaya hiyo ili nao watumie TEHAMA kwa kujiongezea maarifa na uwezo.

Wahitimu 32 walitunikiwa vyeti wakiwamo vijana wajasiriamali 20 kutoka Baraza la Vijana la Wilaya Magharibi A na walimu 12 wamehitimu mafunzo ya TEHAMA ngazi ya awali.



GIGY

UKURASA 12



Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



# MWACHENI AITWE DIAMOND

IMEBAINIKA mwanamuziki nyota nchini, Diamond Platnumz ndiye msanii pekee anayeongoza kuiingizia serikali mapato makubwa kutokana na kazi zake.

Hatua hiyo inakuja baada ya hivi karibuni kukiri kuiingizia serikali kiasi cha shilingi bilioni 1.7 kama kodi kutokana na kazi zake mbalimbali.

Baadhi ya wachambuzi wa sanaa, wanasema Diamond amevunja rekodi ya kuwa msanii wa kwanza anayelipa pesa nyingi kama kodi tangu nchi ipate Uhuru.

Wamesema hatua hiyo imefanikiwa kufika baada ya yeye na timu yake kuamua kugeuza sanaa kama mtambo wa kuingizia fedha, badala ya kuifanya sehemu ya tambo na majigambo.

Christopher  James, amesema hatua aliyofikia mwanamuziki hiyo inafaa kuigwa na wasanii wengine ambao wamebaki kujigamba kwa maneno na kuacha kufanya kazi.

"Tumesikia jinsi Diamond alivyosema kwamba analipa kodi zaidi ya bilioni moja, haya ni mafanikio makubwa na inawapasa kila msanii kuiga na kuachana na tabia ya kujigamba kuwa na gari zuri au nyumba ambazo pengine hawana," amesema.

Diamond katika mkutano wake na viongozi wa serikali, aliweka wazi kwamba kodi anayolipa kutokana na kazi zake ni shilingi bilioni 1.7 kwa mwaka huu.

Amesema kwa kiwango hicho cha pesa anazolipa kama kodi, mwanamuziki huyo ameweza kujenga shule, zahanati na vituo vya afya nchi nzima.

"Diamond anafurahia kuona kodi yake inajenga shule, zahanati na vituo vya afya, yeye ni miongoni mwa mitambo ya kuingizia fedha serikali na hili ni jambo zuri," ameongeza.

BASI SAWA

## Motra elimu si ugomvi



RAPA Motra The Future, amesema ngoma yake mpya 'Weupe' haikuwalenga kundi la Kikosi Kazi, na kutoa ushauri kwamba muziki huo ni sawa na darasa lazima kila mtu ajifunze vizuri.

Mwanamuziki huyo ameeleza kwamba wimbo wake huo ni kama amewakumbusha Kikosi Kazi kuacha kuwachana wasanii wenzao na watafute njia zingine za kutafuta pesa.

Wimbo wake huo ambao ameuachia hivi karibuni, umeonekana kupendwa na mashabiki wengi na kwenye mtandao wa Youtube, unafanya vizuri.

## Chemical umeacha masomo na kuja Dar?



RAPA wa kike msomi, Chemical, ameacha kwa muda masomo yake ya udaktari kwa ajili ya kuja nchini kufanya kazi maalumu.

Chemical anasoma katika chuo kikuu cha Scotland, na siku chache zilizopita alionekana jijini Dar es Salaam, akishiriki mafunzo ya kulinda utamaduni inayowashirikisha wasanii mbalimbali.

Amesema mafunzo hayo ni matokeo ya utafiti wake ambao aliufanya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kumfanya kuwa mwanafunzi bora na hatimaye kupewa ufadhili wa kwenda Scotland.



## Gigy Money wacha ujipandishe chati

MWANAMUZIKI Gigy Money, amesema hata asipotoa ngoma mpya jina lake pekee linatosha kumpatia umaarufu.

Amesema anamshukuru Mungu kuwa na nyota nzuri kiasi ambacho mashabiki wake wanazidi kwa idadi, kiasi ambacho hata mwenyewe kinamshangaza.

"Tangu nifunguliwe na Basata nimekuwa napata matangazo mengi ya kibiashara, kwa ujumla jina langu haliwezi kupotea, kila siku nazidi kupata umaarufu hata nisipotoa wimbo mpya nitaendelea kupaa," amesema.

# Mfufumo: Mfalme wa mchongo

Na Adam Fungamwango

CHEO hakilazimishwi, bali huja chenyewe jinsi watu wanavyokukubali na kukuona unafaa kuwaongoza. Lakini tumeona hata hapa nchini kuna baadhi ya wagombea ubunge walikuwa wakiuza hadi nyumba zao ili wapate pesa za kufanyia kampeni na kuhonga wapiga kura, pesa, nyama na pombe kwa ajili ya kupata uongozi.

Hata hivyo kuna watu ambao hawakutoa hata senti tano, lakini walikubalika na wapiga kura, wakashinda ubunge.

Leo tutaiangalia filamu iitwayo 'Mfufumo' tuone jinsi baadhi ya watu ambao wanatazamisha uongozi kwa njia yoyote ile, mradi tu wapate.

Imechezwa na wasanii Juma Mbega, Francis Malela, Elizabeth Singu, Happyness Masongo, Yohana Joseph na wengine wengi.

Inaanza kwa kuonyesha, mfalme wa himaya ya Mfufumo alitaka kumuandaa kijana wake kuwa mrithi wake, kwani umri wake unazidi kuwa mkubwa sasa.

Malela ndiyo anaandaliwa kuwa mfalme, naye anaitwa na baba yake kuambiwa atafute mchumba kwanza aoe. Kijana huyo anamtafuta msichana mmoja mrembo aitwaye Nchama ili awe mkewe kabla ya kurithi kiti cha baba yake.

Siku ya harusi, bibi harusi akapotea.

Himaya nzima ikawa na taharuki. Kumbe bibi hatusi alichukuliwa kimiujiza porini. Huko anakutana na mpenzi wake wa zamani Bilal. Kwanza anamuogopa kwa sababu anajua ameshafariki. Bilal anamwambia ni kweli amefariki, lakini mzimu wake bado uko hai. Anamwambia kuwa kifo chake hakikuwa cha bahati mbaya, bali kilipangwa na mfalme wa sasa ili kijana wake Malela arithi kiti cha ufalme.

Mzimu wa Bilal ukamwambia mpenzi wake Nchama kuwa yeye ndiye aliyekuwa mrithi halali, kwani mfalme wa sasa ambaye ni baba yake mkubwa, alikuwa ameushikilia kwa muda baada ya baba yake mzazi kufariki. Na kwa sasa imefika zamu ya kulipiza kisasi. Bilal anamchukua Nchama na kwenda naye hadi kwenye harusi ambako walikuwa wanamtafuta.



Radi kubwa ikapiga, watu wote wakatawanyika. Ikawa ni hofu kubwa kijijini. Mfalme akaanza kuugua ugonjwa usiojulikana.

Mfalme ilibidi awaite wazee na kuwaeleza ukweli kuwa, alimuua mdogo wake ambaye alikuwa mfalme na kwa sababu mtoto wake Bilal alikuwa mdogo ilibidi arithi yeye kaka mtu hadi Bilal atakapokuwa mkubwa. Lakini hata alipokuwa mkubwa, akamuua na Bilal ili mtoto wake Malela ndiyo awe mrithi. Baada ya kueleza ukweli wote, 'mfalme wa mchongo' akafariki dunia.





## Rosa Ree tutajie jina basi

MASHABIKI wa muziki wa Bongo Fleva, watarajie kuanza mwaka mpya 2022, na albam mpya ya rapa mkali wa kike, Rosa_Ree, ambayo ipo hatua ya mwisho kukamilika.

Mwanamuziki huyo ameandika katika ukurasa wake wa Instagram akiwataka kila mtu kuwa tayari kusikiliza kazi yake hiyo mpya.

Hata hivyo, Rosa Ree hajataja jina la Album hiyo ,idadi ya nyimbo zinazopatikana na wasanii aliowashirikisha.

# UHURU, WANAMUZIKI MIKONGENI TANGA

Na Adam Fungamwango

KABLA hata ya Uhuru wa Tanganyika, kwa sasa Tanzania Bara, sehemu za Tanga kuanzia Hale kuelekea Tanga mjini kulikuwa na mashamba makubwa ya mkonge ambayo yalihitaji wafanyakazi wengi.

Watu kutoka mikoa mbalimbali nchini walimiminika mikongeni kwa ajili ya kufanya kazi kwenye mashamba hayo. Kutokana na hali hiyo kulihitajika huduma za jamii kama zahanati, shule, baa na hata kumbi za burudani.

Hiyo ilisababisha wenye vipaji vya kupiga magita na kuimba, kutengeneza makundi ya kuburudisha na ndipo kulipoanzishwa makundi kama Atomic Jazz na Jamhuri Jazz ambayo awali ilijulikana kama Nyamwezi Jazz kutokana na wamiliki wa bendi kuwa ni watu kutoka Tabora.

Baada ya Uhuru mwaka 1961, majina yaliyoonekana ni ya kikabila yalipigwa marufuku na ndipo Nyamwezi ilipobadilishwa jina na kuitwa Jamhuri Jazz Band.

Wenye vipaji vya muziki, pamoja na kuburudisha wenzao, waliwafundisha watoto muziki, hivyo kutengeneza kizazi cha wanamuziki baada ya watu hao waliahamia.

Wazee hao walioangozwa na Mwanamasongi, walitengeneza vijana wengi waliokuja kuwa wanamuziki wakubwa nchini na Afrika Mashariki.

Hawa ni baadhi ya wanamuziki wakubwa tu ambao wametokea Tanga, na asili ya wazazi wao ni watu waliokuja kwenye kazi za mikonge.

**Wilson Peter na Geoge Peter Kinyonga**

Wanamuziki hawa ndugu ni baadhi ya wanamuziki ambao wametokea maeneo ya Hale mkoani Tanga.

Asili yao ni mkoa wa Kigoma na Rukwa walikotokea wazazi wao wakija kufanya kazi mikongeni.

Walitokea kuwa wanamuziki wakubwa Afrika Mashabiki, baada ya kuunda bendi ya Simba Wanyika nchini Kenya.

Kabla ya hapo walianzia Tanga kwenye bendi ya Jamhuri Jazz kwenye miaka ya '60, kabla ya kuelekea Arusha na kuvuka mpaka kuelekea Kenya ambako walipiga muziki kwa miaka mingi, wakafariki huko na kuzikwa huko mwanzoni mwa miaka ha '90.

**Tx Moshi William**

Ukimsikiliza Tx Moshi uimbaji wake, unafanana sana na George Peter wa Simba Wanyika. Ukweli ni kwamba Tx Moshi alimpenda sana mwanamuziki huyo na kuiga aina yake ya uimbaji.

Kwa mujibu wa Tx Moshi mwenyewe kabla hajafariki mwaka 2006, ni kwamba alicheza na George wakati wa utoto, huku Wilson akiwa mkubwa kidogo kwao.

Na wote walifundishwa muziki na mzee Mwanamasongi huko Hale mkoani Tanga.

Kwa upande wake wazazi wake walitoka Mwanza na mama yake akitokea Ruvuma.

Baada ya kutoka mkoani Tanga, alikwenda Dar es Salaam na kujiunga na Polisi Jazz, kabla ya kuchukuliwa na Juwata Jazz Band 'Msondo Ngoma'.

**Hamza Kalala**

Ni mpiga solo maarufu nchini. Wazazi wake wana asili ya mkoa wa Katavi kwa sasa.

Walikwenda Tanga kwa sababu ya kazi za mikonge. Yeye amezaliwa huko na kujifunza muziki, kabla ya kuwa mwanamuziki mkubwa nchini, akipigia bendi mbalimbali kama Uda Jazz, Vijana Jazz, Matimila, Washirika na Bantu Group.

**Hemed Maneti**


Ni mwanamuziki mwimbaji maarufu nchini aliyefariki dunia mwaka 1990 jijini Dar es Salaam akiwa ni kiongozi wa bendi ya Vijana Jazz.

Huyu naye ametokea mikongeni Tanga. Baba yake ni mzaliwa na Sumbawanga mkoani Rukwa na alikwenda huko na kufanya kazi ya udereva.

Alifundishwa muziki huko, lakini aliibukia mkoani Morogoro akiwa na Cuban Marimba, TK Lupopo na baadaye Vijana Jazz.

**Luza Elias**

Huyu ni mpiga saxophone maarufu nchini akitokea mkoani Iringa. Aliibuka kuwa mwanamuziki maarufu akiwa na bendi ya Jamhuri Jazz akiwa na kina Wilson Peter na George Peter na baadaye walimchukua kwenda naye Simba Wanyika, kabla ya kurejea nchini na kujiunga na Mwenge Jazz.



# Nick yote mapenzi ya Mungu

MWIGIZAJI na mtanagazaji wa televisheni, Nick Cannon, yupo katika majonzi mazito baada ya kumpoteza binti yake mdogo, Zen.

Staa huyo alionekana akitokwa na machozi mbele ya watazamaji wakati akiendesha kipindi chake.

"Nina huzuni kupitia wakati huu, ninachoweza ni kumshukuru Mungu, watu wananiambia niombe kupata maajabu ya Mungu, lakini nipo pamoja naye daima," amesema.



## Lil Wayne kwa nini utoe bunduki?

RAPA maarufu wa Marekani, Lil Wayne  anakabiliwa na uchunguzi wa polisi baada ya kudaiwa kuwatolea bunduki walinzi.

Kulingana na mtandao wa TMZ, mwanamuziki huyo na mlinzi mmoja wa usalama walijikuta wakijibizana maneno na baadae ikazuka vurugu kubwa iliyosababisha kujibizana kwa risasi.

"Tumeambiwa walinzi walimlalamikia Wayne kwa kukataa kutoka ndani ya nyumba, lakini alikwenda bafuni na huko kukaendelea majibizano makali," amesema mtoa taarifa.


## Beverly wape maneno yao

MSANII wa filamu kutoka Nollywood, Beverly Naya, amesikitishwa na baadhi ya nchi za Kiafrika kuwekewa karantini ya usafiri kwa sababu ya kuibuka kwa virusi vipya vya Omicron.

Kupitia ukurasa wake wa Twitter, Naya amesema inatia wasiwasi kutokana na nchi za Ulaya kuwatizama vibaya Waafrika kama wao ndio chanzo cha corona.

"Nimevunjwa moyo kila wakati kusikia Waafrika wanazungumzwa vibaya kwamba bara letu linawahitaji nchi za Magharibi, hili jambo baya sana hasa kutuwekea zuio eti kwa sababu ya Omicron," amesema.





## Wadude aitamani Zanzibar

MSANII kutoka Nigeria, maarufu kama Wadude, amefanya maajabu baada ya kuachia ngoma yake mpya inayoitwa Zanzibar.

Wimbo huo ambao umewashangaza mashabiki wengi, ni baada ya video ya ngoma hiyo kuonyesha mandhari ya Zanzibar.

Wadude amesema wimbo huo ameutunga baada ya kufanya Safari yake ya Zanzibar kama matembezi.

## Princess huyo mtu nani?

MWIGIZAJI kutoka Ghana, Princess Shyngle, ambaye anasifika kwa vituko vyake, amewaacha mashabiki wake njia panda baada ya kumtaja kiaina mwanaume mmoja mwenye jinsi mbili.

Katika ujumbe wake kupitia ukurasa wa Instagram, Princess Shyngle amefichua kuwa mwanamume huyo ambaye anapenda starehe, mwenye umri wa miaka 35 anajulikana kuwa tapeli.

"Mwanaume yeyote narudia tena mwanaume yeyote ambaye anafanya vizuri maishani, anastarehe na 35 hapo juu lakini hajaoa anabadili wanawake kila dakika kama suruali ni mwanaume mwenye jinsi mbili," ameandika.



# MNUFAIKA TASAF:
# Kutoka kulima vibarua hadi mageuzi ya kumiliki mifugo

## ●Ashauri wanaofanyia anasa fedha za TASAF...

**Na Beatrice Bandawe**



ALICE Mtunga akihudumia mifugo yake nyumbani kwake, Kata ya Msaranga, Manispaaya Moshi Mjini. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

ALICE Abakuki Mtunga (74), ni mkazi wa Kata ya Msaranga katika Manispaa ya Moshi Mjini, mkoani Kilimanjaro, anayeishi na mjukuu wake aliyetelekezwa na mtoto wake tangu akiwa na miezi miwili.

Ni kati ya wanufaika wa Mpango wa Kupunguza Umaskini Nchini (TASAF), aliyejikomboa kutoka kufanya vibarua vya kulima mashamba ya watu mpaka kuwa mfugaji.

Mjukuu wake, Clinton Gabriel ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 20, alitelekezwa kwa bibi yake bila kupata msaada wowote kutoka kwa wazazi wake na kulelewa na bibi huyo kwa kutegemea vibarua vya kulima mashamba ya watu.

Mazingira ya umaskini aliyokuwa akiishi nayo na mjukuu wake, ndiyo yaliyomfanya atambuliwe na kuingizwa kwenye mpango huo wa kupata ruzuku ya TASAF.

Beatrice Kimario, Ofisa Mtendaji wa kata hiyo, anasema eneo lake lina walengwa 64 kwenye mpango huo.

Alice aliingia katika mpango wa TASAF kwa kupata ruzuku ya Sh. 20,000 na hupokea kila baada ya miezi miwili.

“Nilipoingizwa kwenye mpango nilianza kupokea Sh. 20,000 ambazo ziliniwezesha kununua vifaranga vya bata watatu nilioanza kuwafuga na kufikisha bata 30,” anasema Alice, akiwa na uso wa furaha.

Anasimulia kabla ya mpango huo, alikuwa akifanya kazi ya vibarua kwa kulima mashamba ya watu na kupata fedha ya kula na mjukuu wake.

“Maisha yalikuwa magumu sana, wakati mwingine hata mlo mmoja tunashindwa kuupata, lakini fedha hizi za TASAF zimenisaidia sana naendelea kufuga na mifugo mingine nauza,” anasema.

Mtoto wake alimtelekezea mjukuu huyo bila kumpa msaada wowote na tangu alipoondoka hajawahi kurudi kumuona mtoto wake wala mawasiliano ya simu.

Kupitia bata anaofuga, anasema wamemuongezea kipato na mifugo mingine ikiwamo nguruwe na mbuzi.

Licha ya umri alionao, Alice pia anajishughulisha na kilimo kwa kukodi shamba lenye ukubwa wa heka moja analolima mahindi na kumwezesha kuvuna magunia 10.

Kupitia fedha anazopata kutoka kwenye mifugo na mazao anayouza, ameweza kumsomesha mjukuu wake katika chuo cha ufundi na sasa anajitegemea.

“TASAF imetusaidia sana hasa sisi wazee vikongwe natamani iendelee kuwapo na kuendelea kutusaidia, lakini kwa sababu na wengine wanataka kunufaika sina jinsi,” anasema.

Hata hivyo, anasema hata akiondolewa atabaki na amani kwa sababu anaweza kumudu maisha kutokana na shughuli zake za ufugaji.

“Wanaotumia vibaya pesa za TASAF kufanya anasa mimi naona ni wapuuzi, nashauri ikiwezekana wapewe adhabu kali, huu mpango umetutoa katika lindi la umaskini,” anasisitiza.

Jolenice Bahati Ngowi (70), ni mjane anayeishi kata hiyo ya Msaranga, ambaye pia ana wajukuu kadhaa anaowalea baada kutelekezwa na watoto wake.

Aliingizwa katika mpango huo kwa kupata ruzuku ya Sh. 32,000 anayoipata kila baada ya miezi miwili.

“Ruzuku ya TASAF imenisaidia kupata cheti kinachoniwezesha kupata matibabu,” anasema Jolenice, ambaye anafafanua kuwa awamu ya pili ya fedha hizo ilimsaidia kununua mbuzi wa kufuga.

Anasema mbuzi wake alipozaa, alimuuza jike moja na kununua dume ili kuongeza idadi ya mifugo.

“Mifugo ilipoendelea kuzaliana nikasema sasa ni wakati wa kulala mahali pazuri, nikauza baadhi nikanunua godoro zuri na sasa nalala usingizi mzuri,” anasema.

Hata hivyo, anasema hakuridhika na maisha hayo, aliendelea kuongeza vyanzo vya kumpatia fedha kwa kukodi shamba ambalo analima mahindi na kumpatia kipato.

Anasema kitu kikubwa anachoshukuru kupitia mpango huo ni kumwezesha yeye na wajukuu wake kuishi vizuri na kupata chakula ambacho hapo awali ilikuwa ni tatizo.

Pia, anasema wajukuu zake sasa wanaweza kwenda shule bila usumbufu wa kurudishwa nyumbani kwa kukosa sare kwa sababu ya ruzuku hiyo ya TASAF, lengo lake pia ni kusaidia watoto walio kwenye kaya maskini kuwezeshwa kwenda shule na kupata vifaa muhimu.

“Kikubwa ninachoshukuru pia ni kupata bima ya matibabu mimi na wajukuu zangu,” anasema Jolenice.

Hata hivyo, ameshauri kutolewa elimu ya kutosha kuhusu matumizi ya fedha hizo za ruzuku kutokana na baadhi kutumia vibaya kinyume na malengo yaliyowekwa.

“Wale wasioendeleza pesa za TASAF inabidi wapewe elimu na wasipotumia kwa lengo lililowekwa wanyimwe,” anasema.

Mpango wa TASAF awamu ya tatu ulikuwa na lengo la kuwezesha kaya maskini kuongeza kipato kwa njia endelevu na kuwekeza kwenye rasilimali watu.

Mpango huo una lengo la kuwezesha kaya maskini zilizo katika hali duni ya maisha kujikomboa kwa kuwa na miradi endelevu kupitia ruzuku zinazotolewa na TASAF na hatimaye kujiingiza katika vikundi vitakavyowawezesha kupata mikopo ya riba nafuu.

Mpaka mwaka jana, jumla ya vikundi 13,426 vyenye wanachama 187,560, viliingia katika mpango wa kuweka akiba na kukopa, kati yao 876 ni kutoka visiwani Unguja na Pemba.

Mtaalam wa Mawasiliano wa TASAF, Zuhura Mdungi, anasema, lengo la mpango huo ni kuhakikisha wanufaika wanatumia ruzuku walizopewa kufanya miradi endelevu, ili waweze kujiendesha wenyewe bila kutegemea ruzuku hiyo.

“Tunataka kuona walionufaika wanatoka kwenye mpango ili kaya zingine maskini nazo ziweze kuingizwa na kufanya miradi endelevu,” anasema.

Madhumuni ya kipindi cha pili ni kuongeza fursa za kujiongezea kipato na kuboresha huduma za kiuchumi na kijamii kwa kaya za walengwa na kulinda maslahi ya watoto wao.

Kipindi cha pili cha TASAF kitafikia malengo yake kwa kutekeleza shughuli mbalimbali kupitia sehemu kuu tatu ambazo ni uhawilishaji fedha utakao ongeza kipato cha kaya na kuwekeza katika afya na elimu ya watoto, kuinua uchumi wa kaya kwa kujenga uwezo wa utunzaji rasilimali na kutengeneza njia mbadala na endelevu za ajira na kushiriki katika kazi za jamii za kupata kipato cha ziada kwa matumizi ya kaya kama chakula na kugharamia mahitaji mengine ya msingi.



## TULIKOTOKA, TULIKO & TUNAKOELEKEA...

# Uhuru na Taifa Cup: Mkongwe wa 1964 aliyeibua vipaji lukuki



**Na Adam Fungamwango**

MNAKAA kwenye redio, mtangazaji anasema "Sasa tunawapeleka kwenye Uwanja wa Karume Jijini Dar es Salaam kusikiliza maelezo ya mpira wa miguu, michuano ya Taifa Cup, leo ni kati ya timu ya mkoa wa Dar es Salaam 'Mzizima United' na timu ya mkoa wa Dodoma, 'Mazengo Warriors'.

Hiyo ilikuwa ni miaka ya nyuma, wakati huo michuano ya Kombe la Taifa, ikiwa iko juu. Ilikuwa ni michuano maarufu zaidi nchini Tanzania ukiondoa Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara ambayo ndiyo hii ya Ligi Kuu.

Hii ndiyo michuano mikongwe zaidi kuliko hata Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo ilianza mwaka 1965, miaka minne baada ya Uhuru.Michuano ya Taifa Cup ilianza mwaka 1964. Kabla ya hapo ilikuwa chini ya wakoloni ambao walikuwa wakiita Sunlight Cup. Ni michuano ambayo ilikuwa inazishirikisha timu za mikoa. Mikoa yote Tanzania ilikuwa ikiunda timu ya soka na kushiriki michuano hiyo ambayo ilijizolea mashabiki wengi.

Taifa Cup, ni michuano ambayo ilitoa wachezaji wengi ambao walikuja kuzichezea klabu kubwa za Simba na Yanga.

Klabu hizo zilikuwa zikiifanya michuano hiyo kama kioo chao cha kutafuta wachezaji wa kuwasajili.

Na kweli, ilikuwa ni michuano iliyokuwa ikikusanya vipaji vingi kutoka kila kona ya nchi na kuiweka sehemu moja, ikawa ni rahisi tu kwa klabu zinazotaka wachezaji kuwachukua.

Uzuri wa michuano hii ilikuwa inaleta wachezaji kutoka ndani kabisa vijijini na kuwapeleka mjini ili kuonyesha vipaji vyao.

Mchezaji ambaye ana kipaji alikuwa akifika Dar, harejei tena mkoani. Anasajiliwa na klabu za Dar, kazi imekwisha.

Mfano kama ni mkoa wa Tabora unatafuta kikosi cha mkoa huo. Viongozi wa chama cha soka wanazunguka mijini na vijijini kusaka vipaji, au wanaanzisha mashindano kwa klabu mbalimbali za mijini na vijijini. Wachezaji walioonyesha uwezo na wenye vipaji, huchukuliwa kutengeneza timu ya mkoa huo, baadaye wakati wa kwenda kucheza Taifa Cup, timu inachujwa na inayobaki inapelekwa kwenye michuano.

Ndiyo maana michuano hiyo ilikuwa inawawezesha hata wachezaji kutoka vijijini kuonekana. Wengine unaweza kukuta walikuwa hawajawahi kuishi hata Tabora mjini, lakini anapata nafasi ya kutoka labda Usoke na kwenda moja kwa moja Dar es Salaam ambako mara nyingi ndiyo ilikuwa ikifanyikia michuano hiyo.

Na kweli, mchezaji mwenye kipaji atasalia Dar tu. Taifa Cup mara nyingi ilikuwa ikichezwa kwenye Uwanja wa Karume jijini Dar es Salaam, awali ikijulikana kama Ilala Stadium.

Wachezaji bora wote kutoka pande zote za Tanzania walikuwa wanakusanyika sehemu moja kuonyeshana jinsi soka linavyosakatwa.

Hata hivyo, historia ya michuano hiyo inasema kuwa Dar es Salaam ndiyo imechukua kombe hilo mara nyingi zaidi, ikiwa imetwaa mara 12, tangu mwaka 1964 hadi ilipokomea mwaka 2011. Na ukiangalia sababu si tu kwamba michuano hiyo mara zote ilikuwa inachezwa Dar tu, ila kila mwaka inapochezwa michuano hiyo, baadhi ya wachezaji wanabaki Dar kwa kujisajili na Simba au Yanga Cosmopolitan kwa hiyo mwaka unaofuata wanakuwa wana sifa za kuichezea timu ya mkoa wa Dar na si mikoa waliyotoka tena. Ni kwa sababu moja ya kanuni ya michuano hiyo ni kwamba mchezaji anatakiwa achezee mkoa anaoishi au klabu anayochezea.

Ni wachezaji wengi sana ambao michuano hiyo iliwatoa na kuonekana na klabu za Simba na Yanga ambao ukiwaandika hapa majina yao hawatoshi

Na wachezaji walionufaika zaidi ni kutoka Morogoro, Tanga, Kigoma na Mwanza kidogo. Hiyo ndiyo mikoa iliyokuwa ikizalisha vipaji vingi na kuilisha Dar es Salaam ambayo ikawa inawatumia kwenye michuano hiyo wanapohamia Dar.

Kati ya mara hizo 12, mara nne ilikuwa ikiitwa Pwani, ambapo mkoa ulikuwa haujagawanyika, kwani Dar es Salaam ilikuwa ndani ya mkoa wa Pwani. Baadaye jiji la Dar likawa mkoa, na Pwani ikaachwa peke yake bila Dar.

Mikoa ya Morogoro na Mwanza inashika nafasi ya pili kwa kulitwaa kombe hilo mara mbili kila moja, Moro ikilitwaa kombe mwaka 1970 na 1974, huku Mwanza ikilichukua mara mbili mfululizo mwaka 1984 na 1985

Kwa sasa inaonekana kabisa kuwa imekufa kabisa. Ilianza kukosa nguvu, baada ya kanuni nyingi kuongezwa, Dar ikagawanyika zikawa timu tatu za Ilala, Temeke na Kinondoni. Lakini pia ikatengenezwa kanuni kuwa kila mkoa uchezeshe wachezaji watano tu wa Ligi Kuu. Hii ni baada ya mikoa mingi kuacha kuzalisha au kutokuwa na wachezaji wengi wenye vipaji.

Michuano hii iliyoanza mwaka 1964, ilivutia mashabiki wengi waliokuwa wakijazana Ilala, wengine wakisikiliza kwenye redio ambapo kila mwaka Dar ilikuwa ikipata shida licha ya kubakisha mastaa, lakini mwakani, timu za mikoa zinakuja na wachezaji wengine wazuri kuliko wale. Lakini nao wanabaki tena.

Burudani nyingine ilikuwa ni majina ya timu hizo za mikoa, ambapo timu ya mkoa wa Dar es Salaam ilijulikana kama Mzizima United, ya mkoa wa Arusha ilijulikana kama Meru Warriors, Dodoma yenyewe ilikuwa inaitwa Mazengo Warriors.

Timu ya mkoa wa Iringa yenyewe ilijulikana kama Ruaha Star na ile ya mkoa wa Lindi ilifahamika kwa jina la Ilulu Stars na majirani zao timu ya mkoa wa Mtwara iliitwa Mabibo Stars.

Ile ya mkoa wa Kigoma iliitwa Kigoma Stars na timu ya mkoa wa Kagera ilijulikana kama Lweru Eagles, ya Mbeya iliitwa Mapinduzi Stars, na Mwanza yenyewe ni Mwanza Herroes.

Tabora ilijulikana kama Mashujaa wa Unyanyembe, na Shinyanga ni Igembe Nsabo. Morogoro iliitwa Moro Stars na Tanga iliitwa hivyo hivyo, Tanga Stars.

**Meseji simu: +255 0716 350534**

## MIAKA 60 YA UHURU

# Posta ilivyogeuka kuwa ya kidijitali

**Na Mwandishi Wetu**

KUTOKANA na mabadiliko mbalimbali ya teknolojia yaliyoikumba sekta nzima ya posta duniani, Shirika la Posta Tanzania kwa kushirikiana na mashirika mengine ya kiposta, yalianza kuiona teknolojia kama fursa maridhawa ya kubadili kabisa uendeshaji wake sambamba na majukumu yake ya msingi.

Kaimu Posta Masta Mkuu, Macrice Mbodo (pichani), anasema kutokana na mabadiliko hayo, Shirika la Posta la sasa limefikia hatua ya kuwa la kidijitali kutokana na kuanza kutoa huduma zake kwa njia za teknolojia mpya.

Pamoja na hayo, shirika limeanzisha mfumo wake jumuishi unaojulikana kama Postal Management Information System (PMIS) ambapo ndani yake kuna mifumo mbalimbali kama mfumo wa kusimamia rasilimali watu, fedha, uendeshaji wa huduma za posta uliounganishwa (integrated) na wa kimataifa yaani International Postal System na kaunta uliounganishwa na ule wa kimataifa yaani International Financial System, huduma ya EMS.

Anasema mfumo wa kufuatilia mienendo ya barua, vipeto na hata vifurushi vya kitaifa na kimataifa yaani truck and trace pamoja na huduma kwa wateja pia imefanyiwa kazi kidigitali.

Sambamba na uendeshaji wa huduma za posta za kidijitali, Posta ya kidijitali ya Tanzania imeanzisha Duka la Mtandao (e-shop) ambapo wafanyabiashara huingiza bidhaa zao humo na wanunuzi huagiza baada ya kuziona kwenye mtandao, huagiza kwa njia za kidijitali na kufanya malipo kwa njia za kidijitali na baadaye bidhaa walizonunua kwa njia za kidijitali hupelekwa popote walipo kwa njia ya posta ya kidijitali.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, analipongeza Shirika la Posta Tanzania kwa mageuzi ya teknolojia linayoendelea kuyafanya.

Akizindua huduma ya shirika hilo ijulikanayo kama 'Huduma Pamoja', Waziri Mkuu alisema jijini Dar es Salaam kuwa huduma hiyo ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan yenye kuakisi Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 na kwamba ni utekelezaji wa Mradi wa Kitaifa wa Kidigitali.

Waziri Mkuu alisema hatua hiyo itaondoa usumbufu, hivyo wananchi hawatalazimika kutembea umbali mrefu kutafuta huduma za serikali ambazo zote zitapatikana kupitia Huduma Pamoja ya shirika hilo.

Juma Ali, ni mkazi wa Tabata jijini Dar es Salaam, analipongeza Shirika la Posta kwa huduma zake mbalimbali za kidigitali ambazo anasema zitasaidia kuboresha maisha ya wananchi.



"Kwa kweli Shirika la Posta limefanya mageuzi makubwa sana hasa kwa upande wa kidigitali, nalipongeza kwa ubunifu huo," anasema.

Kaimu Posta Masta Mkuu anasema mifumo hiyo pia imetengenezewa 'APP' ambapo mteja mwenye simu janja anaweza kuipakua kwenye simu yake na kuanza kijipatia huduma pasipo kulazimika kusafiri wakati mwingine umbali mrefu kufuata huduma za kiposta kwenye ofisi za Posta.

Mbodo anasema kutokana na hilo, masanduku yale ya zamani yaliyopo kwenye majengo ya ofisi za posta yamewekewa utaratibu wa aina nyingine ambapo namba ya simu ya mtu inaweza kusajiliwa na kuwa sanduku lake la kidijitali.

"Mteja wa namna hii anayo faida ya kupata ujumbe mfupi wa maandishi kwenye simu yake yaani SMS pindi atumiwapo kitu au bidhaa yake kupitia Posta na anaweza kufuatilia bidhaa yake kupitia simu yake.

"Bidhaa husika ikifika kwenye ofisi ya Posta, SMS hutumwa kwenye simu ya mkononi na yeye mwenyewe huchagua njia ya kufikishiwa kitu chake, aidha aje ofisi za Posta kuchukua mwenyewe au apelekewe mahali popote alipo au atakapo," anasema.

Anasema Mtanzania akiingia ndani ya ofisi za Posta hahitaji kuanza kusumbuka huku na kule kutafuta ofisi zingine za kiserikali bali huhudumiwa ndani ya ofisi moja kirahisi na kwa wakati.

Mfano mtu anayehitaji hati ya kusafiria (Passport) akifika ofisi za posta atafanya taratibu za Idara ya Uhamiaji, kama hana Kitambulisho cha Taifa (NIDA) atafanya taratibu za kupata kitambulisho cha taifa humo humo bila kutoka na kama kuna malipo atafanya taratibu za malipo humo humo ndani ya ofisi za posta.

"Hati yake ya kusafiria ikiwa tayari anaweza pia kupelekewa kule atakako yeye kwa njia za kiposta," anafafanua.

Anasema Shirika la Posta Tanzania la kidigitali kwa ujumla limerahisisha sana huduma za kiposta tofauti kabisa na nyakati za baada ya uhuru wa Tanzania Bara.

Anasema huduma zilikuwa zinachukua muda mwingi kwa kuwa wafanyakazi walikuwa wakichukua nyaraka za posta kwa miguu.

"Posta ya kidigitali ya leo ni kubofya tu kupitia mifumo wezeshi iliyofungwa na haina usumbufu na ni salama kwa kuwa hata ofisi za posta ya kidijitali kwa sasa zina usalama wa kidijitali kupitia kamera za CCTV zilizofungwa kwenye majengo ya Posta yaliyo na mwonekano mpya wa kidijitali," anatamba.

**POSTA KABLA YA UHURU**

Mbodo anasema huduma za Posta kama taasisi zilianzishwa nchini na serikali ya kikoloni ya Ujerumani ambayo ilitawala kwa pamoja nchi za Tanganyika, Rwanda na Burundi. Makao Makuu ya Posta kwa nchi zote hizi yalikuwa katika jengo la Posta ya Sokoine (Posta ya Zamani) jijini Dar es Salaam.

Huduma ya kwanza ya barua iliyobandikwa stempu ilianzishwa nchini mwaka 1893 na barua hizo zilitumwa kwa kutumia matarishi waliokuwa wanatembea kwa miguu umbali mrefu kwenye makao makuu ya wilaya na majimbo.

Huduma ya treni kati ya Dar es Salaam hadi Kigoma na baadaye hadi Mwanza na Arusha iliboresha mtandao wa huduma za Posta nchini.

Anasema mnamo mwaka 1951, utawala huo uliunda chombo cha kusimamia huduma za pamoja katika nchi za Tanganyika, Kenya na Uganda yaani East African Common Services Organisation (EACSO).

"Chini ya Umoja huo ilitungwa sheria ya kuanzishwa taasisi ya Posta na Simu ya Afrika Mashariki (EAPTA) ambayo iliendelea kusimamia huduma hizi hadi wakati wa Jumuiya ya awali ya Afrika Mashariki mwaka 1967," anasema.

**POSTA BAADA YA UHURU**

Anafafanua kuwa mara baada ya Uhuru wa Tanzania Bara Desemba 9, 1961, huduma za Posta ziliendelea kusimamiwa chini ya sheria iliyoanzisha Taasisi ya EAP&TA.

"Pamoja na mambo mengine taasisi hii ndiyo iliyokuwa na mamlaka pekee na kamili ya kusimamia na kutoa huduma za posta katika nchi za Kenya, Uganda na Tanganyika.

"Mara baada ya uhuru taasisi ya EAP&TA iliendelea kuwa chini ya bodi iliyokuwa inaundwa na wajumbe wa nchi zote tatu," anasema.

Ofisa Mtendaji aliendelea kuwa Postamasta Mkuu, ambapo chini yake walikuwako wakurugenzi wa mikoa ya kiposta wa nchi za Kenya, Uganda na Tanganyika. Makao makuu yalikuwa Nairobi, Kenya ambapo ofisi kuu ya mkoa wa Tanganyika ilikuwa Dar es Salaam katika jengo la Posta la Sokoine.

**SHIRIKA LA POSTA**

Anasema kutokana na kusambaratika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Serikali ya Tanzania iliteua kamati ya kuandaa sheria ya kuunda Shirika la Posta na Simu Tanzania ili kuchukua nafasi ya Shirika la Posta na Simu la Afrika ya Mashariki.

Anasema shirika jipya liliundwa kwa Sheria ya Bunge Na. 15 ya mwaka 1977 iliyoanza kutumika rasmi Februari 3, 1978. Muswada wa kutunga sheria hiyo uliwasilishwa bungeni na Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Amir Jamal, ambaye pia alisimamia huduma nyingine zilizojumuishwa chini ya Jumuiya ya Afrika ya Masharikі kama reli, bandari, ndege, usalama wa anga na hali ya hewa.

Kutokana na kupitishwa kwa sheria hiyo, Rais Julius Nyerere alimteua aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara mbalimbali, Fredrick Mchauru, kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa kwanza na William Maeda ambaye alikuwa Katibu wa Kampuni ya Simu za Nje ya Afrika Mashariki kuwa Mkurugenzi Mkuu wa kwanza wa shirika hilo.

Shirika la Posta Tanzania lilianzishwa kwa Sheri Na. 19 ya Mwaka 1993 baada ya kurekebishwa kwa lililokuwa Shirika la Posta na Simu Tanzania (TP&TC). Shirika hilo lilianza Januari Mosi 1994.

Shirika la Posta linamilikiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100 na liko chini ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA INAUZWA.

NYUMBA YA GOROFA INAUZWA IPO UKONGA,INAFREM NANE ZOTE ZINA WAPANGAJI,INAFAA KWA MAKAZI AU BIASHARA,BEI MAELEWANO(WAWEZA LIPA KWA AWAMU) **SIMU.0715 244754**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0782253676

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/84)**
**Mahakama ya mwanzo ya KAWE**
**Wilaya ya KINONDONI**
**Madai nambari 18 ya 2021**
**Mdai……………FREDY JAMES IRENGE**
**Amdai**
**BRUNO FREDRICK MATUTU**

Kwa **BRUNO FREDRICK MATUTU WA DAR ES SALAAM**
Kwakua mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba

**UNATAKIWA KUFIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA SIKU YA TAREHE 16/12/2021**

Kwahiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya …….tarehe 16/12/2021 saa 2:30 asubuhi kwakujibu madai haya.nakwakua siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wake/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo
Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu,mahakama ikithibitika kama umepokea kuitwa shaurini hii,itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa
Hati hii yatolewa kwa mari yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 12/11/2021

**IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**TEMEKE HIGH COURT SUB-REGISTRY**
**(ONE STOP JUDICIAL CENTRE)**
**AT TEMEKE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 37 OF 2021**

In the matter of the estate of the late WILBAD TEWELI MWORIA and in the matter of of an application for letters of administration by

ADELINA INNOCENT JESUIT MACHA…..1ST PETITIONER
LADISLAUS WILBAD TEWELI……….2nd PETITIONER

GENERAL CITATION
(RULE 75)

All perasons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant letters of administration is made to the above named petitioner

Objections to the grant should be filed on or before the 16th day of December,2021

**Dated at this 30th day of November,2021**

DEPUTY REGISTRAR

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BRAEBURN SCHOOL (T) LIMITED** inatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA IST** yenye namba za usajili **T 557 DMU**,chasis namba **NCP605001691**,engine namba **2NZ4308887**,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **ARU/ARU/RB/51259/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya**
**Wilaya ya ………..TANGA**
**Kituo cha….. MJINI TANGA…. Mkoa… TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi…………211…………2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: HUSSEIN HAMISI KILAMA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA**
**MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA: HADIJA MWEDI SAIDI**

**TANGAZO**
***(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)***

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslai yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28/12/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 6/11/2021**

MAHAKAMA YA MWANZO MJINI TANGA
HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO TANGA MJINI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA.**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA BUKOBA HATI YA KUITWA SHAURINI**
**(SUMMONS)**

Shauri la rufaa madai namba 25/2021
mahakama ya wilaya ya Bukoba
Jina VICENT KAJERELO RUTATINISIBWA
Appellant/ Applicant

Dhidi ya

Jina ANGELA WILLISON Respondent
Kwa ANGELA WILLISON popote ulipo.

Elewa kuwa kesi ya rufaa hiyo hapo juu itatajwa tarehe 20/12/2021 asubuhi katika Mahakama ya wilaya ya Bukoba. Hivyo unapaswa kuhudhuria bila kukosa
Hati hii imetolewa na kutiwa mhuri wa mahakama leo tarehe 30/11/2021.

……………………………………
**HAKIMU MKAZI MFAWIDHI**
**MAHAKAMA YA WILAYA YA BUKOBA.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**SAMUEL SIMON RUMITO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne cha shule ya sekondari Kaisho cha mwaka 2008 Index namba **S0586/0132 NA CHETI CHA** Kidato cha sita shule ya sekondari Rulenge cha mwaka **2011** chenye index namba S397-0559 vilivyotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa.Atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.Taarifa ya Polisi ni **KAG/BUK/RB/52127/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BARANDA HUSSEIN HASANI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari lenye namba za usajili **T487DCM** aina Toyota Noah, chasis namba **SR400157487**, Engine namba **3S0445825.** Kwa yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chocolate cha polisi kilichopo karibu naye.
Polisi Taarifa: **MAN/BAB/RB/580301/2021**

## KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**JOHN PHILIP KAPWANI**, Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari, Yenye namba za usajili **T 932 AKA** Chassis namba **LBCAHIAF513419**, Engine namba **9029910E** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi Taarifa: **ARU/MUR/RB/4747463/2021**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO. 188 OF 2021**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**YOWEL NDAMA MTAITI**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATIONFOR LETTERS OF ADMINISTRATION**

**BY SILVANUS YOWEL NDAMA**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES)**

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 15th Day of December, 2021.
Dated at Dodoma this 29th day of November, 2021

……………………………………
**PETITIONER**
**GIVEN under MY HAND and SEAL of this Court this 3rd day of December, 2021**

……………………………………
**MAGISTRATE**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Morogoro**
**Kituo cha BOMA Mkoa wa morogoro**
**Usimamizi wa Mirathi na…1…2021**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU IBRAIM MAJID MKOMWA WA MAGADU MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MAHAKAMA YA MWANZO BOMA.**

**TANGAZO**
(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo **17/12/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia :**
Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehem anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

Imetolewa leo tarehe 16 Mwezi 11 Mwaka 2021

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo kihonda**
**Wilaya ya Morogoro**
**Mkoa wa morogoro**
**Usimamizi wa Mirathi na…7…2021**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU ANTHONY ALIFA CHAMWALI WA KARUME B**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MARTINA NJOHOLE CHAMWALI**

**TANGAZO**
*(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)*
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo 12/01/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia :
Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehem anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

Imetolewa leo tarehe 10 Mwezi 12 Mwaka 2021

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

DIANA ni msichana mrembo kwa maana halisi ya urembo. Na mwenyewe alijijua kuwa ni mzuri wa shani. Aliwababaisha, kuwaliza na kuwatia wazimu wanaume wengi ambao walikutana nao, au hata kupishana tu. Wengi walimkimbilia. Wakamtongoza, kumtaka kimapenzi. Wapo waliotaka kumuoa kabisa. Hata hivyo yeye mwenyewe hakujua ni mwanaume gani anayempenda kwa dhati. Alichojua wengi wanamfuata kama nyuki wafuatavyo ua zuri la waridi. Aliacha muda uongee. Alijua mwisho wa siku atajulikana ni nani anayependa uzuri na urembo wake na nani nampenda kwa dhati. Alayempenda yeye kama yeye na si urembo wake. Fuatilia mtiririko huu wa riwaya hii kabambe, yenye kusisimua na mafunzo kwa jamii.

# Operesheni Namba Moja-4

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Alipora mkoba wa diana na kuanza kukimbia nao.

"Mama yangu weee." Ilikuwa sauti ya Diana ambaye alipigwa kikubwa, mkoba ulikuwa kwenye meza, mwizi alikuwa na shabaha nzuri kwani aliukwapua na kuanza kutimua mbio.

Kitendo bila kuchelewa. Jamaa aliyekuwa anakula na Diana naye alitoka spidi pamoja na mwizi nje. Kitendo kile kiliwachanganya watu wote waliokuwa mle ndani wasijue nini kimetokea. Baadhi walitoka nje kuangalia ni kitu gani kimetokea.

Walichoona ni jamaa kumzidi mbio mwizi, kabla ya kumpiga mtama. Mwizi akaanguka chini. Akachukua mkoba na kumpiga mateke kadhaa kabla watu hawajafika kulizia kuna nini.

"Ni mwizi huyu, kapora mkoba wa dada wa watu wakati anakula pale hotelini," Alijibu.

Kilichofuatia ni kipigo kutoka kwa raia wema.

Jamaa hakuendelea. Alichukua mkoba wake na kumwacha mwizi akiwa mikononi mwa wananchi wenye hasira kali. Akarudi hadi kwenye mgawaha ule. Alimkuta Diana na watu wengine aliowaacha wako nje. Diana alikuwa analia machozi.

"Mkoba wako huu dada."

Diana hakuamini. Alidhani labda anaota ndoto. Kuporwa mkoba na mwizi mwenye mbio kiasi kile, lakini umerudishwa kabla hata dakika 10 hazijapita ni bahati iliyoje.

Alishindwa hata kushukuru. Alibaki anamwangalia tu baba wa watu huku machozi yakiwa yanambubujika kama bomba la mvua.

"Hebu angalia vitu vyako kama vipo vyote. Kama vimepungua nirudi nimfuate."

Diana aliangalia vitu vyake alivyoweka na kukuta vyote viko sawa. Vipodozi na pesa taslim shlingi laki mbili.


"Vipo vyote ahsante sana."

"Haya ahsante dada, sasa kama umemaliza chakula, inabidi uondoke, maana hawa wezi wanakuwa na wenzao, wanaweza kukufuata nyuma nyuma."

"Kweli kaka naomba nisindikize."

"Poa tu."

Diana kwa mara ya kwanza akataka kujua jina la jamaa aliyemlipia chakula na kumkimbiza mwizi aliyepora mkoba wake.




**"Heee, jamani Mungu mkubwa, maana ni kweli ulinipa namba, lakini niliisevu vibaya, nikawa sijui tena namba yako na sikuwa na uhakika wa kuipata tena. Nilihuzunika sana. Nikasema nitampata wapi tena yule dada? Nitapata wapi tena namba yake. Nikaona ndiyo basi tena siwezi kuwasiliana nawe au kukuona tena."**

"Naitwa Januari Kamili, au wengi wananiita Jan Kamili."

"Ahsante sana Jan, sina cha kukupa ila naomba namba yako, nitakutafuta siku nyingine, leo hapa tayari nimeshavurugwa kabisa."

"Najua, hakuna neno dada."

Diana alichukua namba ya Jan na pia Jan naye alichukua namba ya Diana. Usiku mzima hakupata usingizi. Alikuwa akimfikiria kijana yule. Hakujua ni kwa nini. Alionekana ni kijana wa kawaida sana. Lakini mkarimu, ambaye amemlipia chakula na kumsaidia kumkimbiza mwizi aliyepora mzigo wake.

Kwa usiku huo aliwasahau kabisa wanaume wengine wawili ambao alionekana kuwaweka moyoni. Chala na Afande Michael.

*******************************

Ilikuwa siku ya tatu baada ya tukio lile kutokea. Asubuhi akiwa amejipumzisha nyumbani, kwani haikuwa siku ya kazi, alisikia simu inaita. Ni Chala.

"Vipi mrembo, mbona kimya?"

"Naumwa mwenzio?"

"Nini mama?"

"Malaria na UTI?" Alijibu kwa sauti ya chini, akijifanya ana maumivu, huku aking'ong'a, kuonyesha kuwa anaongopa.

"Pole mama, sasa uko wapi?"

"Niwe wapi na kuumwa huku, niko nyumbani. Sina hali mwenzako, ni hamu na vyakula vya uchu, lakini pesa sina."

"Basi sawa mgonjwa, ngoja nikutumie hapo hela ya soda. nilitaka nikuite sehemu tupate chakula cha mchana, kumbe unaumwa?"

"Nitashukuru mpenzi." Alisema na kukata simu.

Dakika mbili baadaye, likaingia salio la shilingi laki moja kwenye simu yake.

Ilipita tena robo saa hivi ikaita tena.

Safari hii hakuwa Chala. Ni afande Michael.

"Hujambo my?"

"Sijambo habari yako?"

"Safi, vipi mbona kimya, mzima kweli wewe?"

"Mzima wapi naumwa mwenzio."

"Nini tena mama?"

"Nimeenda kupima hospitalini, wameniambia malaria na UTI."

"Du pole sana, basi nimekupigia nijue kama utakuwa uko free, basi tukutane pale tulipokutana siku ile."

"Loh, pole sana Michael, siwezi kabisa, maana hata nguvu sina hapa."

"Kula unakula lakini?"

"Mhh, nina hamu ya vyakula vya ndimu ndimu."

Ikasikika sauti ya kicheko kutoka kwa Afande Michael.

"Nawajua nyinyi kinadada, mnapeda sana chipsi na mayai au na kuku, ngoja nikutumie."

"Ahsante sana nitashukuru sana."

Dakika 10 baadaye, kwenye simu ya Diana ikaingia shilingi elfu ishirini. Ukichanganya na laki moja aliyotuma Chala, salio lilisoma laki moja na ishirini elfu. Zote alivuna kutoka kwa wanaume wawili. Chala na Michael.

Bado alijisikia kuna kitu kinamsumbua. Hakuna anaumwa. Alisema hivyo kuwazuia wanaume hao kumwita.

"Yaani hawa wote leo walikuwa wananiita mimi, kwa wakati mmoja, ningeenda wapi na kukataa wapi. Bora nilivyowaambia naumwa." Alijipongeza kwa uongo huo.

Aliichukua simu yake. Sasa yeye mwenyewe alipiga sehemu ambayo anaitaka yeye.

"Hujambo wewe."

"Sijambo nani mwenzangu?"

"Ina maana hukusevu namba yangu mwanamume wewe?"

"Mhhh inawezekana nilikosea kusevu."

"Mbona mimi nimekusevu na sijakosea?"

"Dada'angu wee, mjini hapa, inawezekana nimekosea kwa sababu ya kuwaza mambo mengi kichwani." Ni jibu ambalo nusura limpasue mbavu Diana.

"Naitwa Diana, umenikumbuka?"

"Diana, Diana, Diana, yule ambaye siku ile pale aliporwa mkoba Mwananyamala A?"

"Hujakosea, ndiyo huyo huyo."

"Heee, jamani Mungu mkubwa, maana ni kweli ulinipa namba, lakini niliisevu vibaya, nikawa sijui tena namba yako na sikuwa na uhakika wa kuipata tena. Nilihuzunika sana. Nikasema nitampata wapi tena yule dada? Nitapata wapi tena namba yake. Nikaona ndiyo basi tena siwezi kuwasiliana nawe au kukuona tena."

"Kwa nini, mbona mimi nilichukua namba yako Jan?" Aliuliza Diana, lakini alichosikia ni kicheko kifupi kutoka kwa Jan.

"We huwajui wanawake warembo kama wewe. Yaani achukue namba aanze kukupigia kama ulivyofanya wewe hivyo. Ni nadra sana. Na hii nimeiona kwako tu dada."

"Yaani umenifanyia mema yote yale, halafu nikutupe, hata nisikusalimie?"

"Nakwambia hivi dada'angu, wanawake wengi warembo hata umwokoe kwenye ajali ya ndege, akachukua namba zako, wewe usiwe na za kwake, anaweza hata asikupigie." Ikawa sasa ni zamu ua Diana kuangua kicheko.

"Yaani nimeshangaa kunipigia wakati tayari namba zako nimeshapoteza, vipi kwema huko?"

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# MAKOCHA STARS, UGANDA WAFUNGUKA KIWANGO SAFI

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kuchapwa mabao 2-0 dhidi ya Uganda, Kocha Msaidizi wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Shadrack Nsajigwa amesema kikosi cha Tanzania kilionyesha kiwango kizuri katika mchezo huo wa kirafiki wa kimataifa uliochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi.

Kikosi cha Stars kilichocheza mechi hiyo ya kirafiki ya kusheherekea miaka 60 ya Uhuru hakikuwa na nyota yoyote kutoka klabu za Simba na Yanga.

Uamuzi wa benchi la ufundi la Taifa Stars kutowajumuisha wachezaji kutoka timu hizo kongwe ulitoa nafasi ya klabu hizo kujiandaa na mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajiwa kuwakutanisha leo.

Nsajigwa aliliambia gazeti hili wamebaini kasoro ndogo ndogo, ambazo ziliwaruhusu wageni kupata mabao na vile vile kufanya mashambulizi ya mara kwa mara.

Alisema watakapowaita tena kambini, watayafanyia kazi mapungufu yao kwa ajili ya kuwaimarisha na kuwajenga kwa ajili ya kushindana.

"Tumekiona kikosi chetu, kimecheza vizuri sana kipindi chote cha kwanza na hata cha pili, lakini tulipoamua kufunguka kwenda kusaka bao, ndiyo wapinzani wetu wakatumia mashambulizi ya kushtukiza ili kutuadhibu," alisema Nsajigwa nahodha huyo wa zamani wa Stars na Yanga ya jijini.

Beki huyo wa zamani alisema wamefurahishwa kuona kila mchezaji amejituma kuonyesha anahitaji kuipa mafanikio timu hiyo na hilo ni jambo jema kwa maendeleo ya timu na nchi.

Naye Kocha Msaidizi wa Uganda (Cranes), Moses Basena, amesema walikuwa wanawajaribu wachezaji wao ambao wanatoka katika timu ndogo zilizopo nchini kwao, wakiwaandaa kwa ajili ya michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Basena aliweka wazi wamepata baadhi ya nyota ambao watawaongeza kwenye kikosi cha wachezaji wakubwa.

"Hawa wachezaji unaowaona tumewatoa kwenye timu ndogo ndogo nchini kwetu, mpango wetu ni kuwaandaa kwa ajili ya michuano ya CHAN ambayo inawashirikisha wachezaji wa ndani tu, pia kuanza kuingia taratibu kwenye kikosi chenyewe kikubwa. Stars iliyocheza leo ni nzuri, imekosa bahati na sisi tumetumia udhaifu wao wa kujipanga vibaya wakiwa wanashambulia," alisema kocha huyo wa zamani wa Simba.

Mbali na mechi hiyo, Tanzanite (Timu ya Soka ya Taifa Wanawake ya umri chini ya miaka 20), ilikubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa wenzao wa Uganda katika mchezo wa kirafiki wa kimataifa uliochezwa mapema jioni juzi.

Tanzanite ilitumia mechi hiyo kujiandaa na mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia U-20 dhidi ya Burundi watakayocheza Desemba 18, mwaka huu wakati Uganda wao itawafuata wenzao wa Afrika Kusini.

# Ngome, Cairo hatarini kufungwa

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BODI ya Ligi Zanzibar (ZLB), imesema inaangalia uwezekano wa kuvifunga viwanja viwili vya Ngome na Cairo vinavyotumika katika mechi za Ligi Daraja la kwanza kwenye Kanda ya Unguja kutokana na sababu mbalimbali, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa ZLB, Sheha Mohamed Ali, alisema sehemu ya kuchezea katika Uwanja wa Ngome hairidhishi na hiyo inatokana na kuwapo kwa mashimo yaliyosababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha katika kipindi hiki.

Ali alisema uwanja huo pia umetengeneza mabonde ambayo yanawapa tabu wachezaji na kushindwa kuonyesha viwango vizuri.

"Tayari tumeshakutana na Bridge Star ambao wanautumia uwanja huo katika mechi za nyumbani, na wameridhia uamuzi wa kuwahamishia kwenye uwanja mwingine utakaofaa," Ali alisema.

Kuhusu Uwanja wa Cairo uliopo Kiwengwa na unaotumiwa na African Coast, kiongozi huyo alisema kumekuwa na fujo kwenye uwanja huo kila timu yao inaposhuka dimbani.

"Mara kwa mara mashabiki wa timu hiyo wamekuwa wakifanya vitendo vya utovu wa nidhamu usiostahamilika, hali hii imepelekea Bodi ya Ligi kufikiria kuchukua hatua hiyo ya kuufungia," Ali aliongeza.



Wachezaji wa Ihefu SC ya Mbarali mkoani Mbeya wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi ya Championship dhidi ya Kitayosce unaotarajiwa kuchezwa kesho kwenye Uwanja wa Ally Hassan Mwinyi mkoani Tabora. **PICHA: MTANDAO**

# Samia Taifa Cup kuibeba CHANETA

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA), umesema ushindani unaoonyeshwa na timu za mikoa zinazoshiriki mashindano ya Samia Taifa Cup utawasaidia kupata wachezaji bora kwa ajili ya kuimarisha kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Queens).

Mashindano ya Samia Taifa Cup yameanza kufanyika jijini Dar es Salaam jana kwa kushirikisha michezo ya netiboli, riadha na soka kwa wanawake na wanaume.

Waziri wa Sanaa, Utamaduni na Michezo, Innocent Bashungwa alifungua rasmi michuano hiyo ambayo inafanyika chini ya uratibu wa serikali.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwenyekiti wa CHANETA, Devotha Marwa, alisema ana imani baada ya mashindano hayo kumalizika, Kamati ya Ufundi ya chama hicho itakuwa imepata wachezaji watakaokwenda kuongeza nguvu kwenye kikosi cha taifa.

Marwa alisema mashindano ya Samia Taifa Cup yatawapa mwanga wa kupata vikosi imara ambavyo vitakwenda kuiwakilisha nchi katika michuano mbalimbali.

"Timu zimekuwa na mwamko mkubwa sana, kila moja inapambana na inaonyesha wanahitaji kufanya vizuri, hawataki kuona wanaondolewa mapema katika mashindano, ushindani huo utasaidia makocha wetu kupata wachezaji wazuri watakaounda timu ya taifa bora na imara," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza mwendelezo wa mashindano hayo ni mzuri lakini pia mchanganyiko wa umri uliopo unaongeza hamasa kwa timu yenye nyota wadogo kushindana bila kuhofia chochote.

Netiboli imegawanywa katika makundi sita ambapo Kundi A lina mikoa ya Pwani, Geita, Njombe na Mwanza huku Kundi B likiwakilishwa na Mbeya, Kigoma, Mtwara, Rukwa na wakati Morogoro, Ruvuma, Tabora na Kaskazini Unguja wanaunda Kundi C.

Kundi D liko na wachezaji kutoka Simiyu, Songwe, Arusha na Iringa, Kundi E lenyewe lina Kaskazini Unguja, Tanga, Magharibi Unguja, Dar es Salaam na Dodoma, Lindi, Kagera na Kaskazini Pemba wako Kundi F.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### FODEN GHALI ULAYA

KIUNGO wa kati wa Manchester City na England, Phil Foden mwenye umri wa miaka 21, thamani yake ni pauni milioni 128 na ni miongoni mwa wachezaji ghali zaidi duniani. ***(Mail)***

### CHELSEA YAMSUBIRI RUDIGER

REAL Madrid wana matumaini beki wa Chelsea na Ujerumani, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 28 atakubali mkataba na klabu hiyo katika dirisha la uhamisho la Januari na kujiunga nao katika uhamisho wa bila malipo msimu ujao. ***(The Athletic)***

### CASEMIRO ANUKIA CHELSEA

CHELSEA inajipanga kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Brazil na Real Madrid, Casemiro mwenye umri wa miaka 29. ***(El Nacional)***

### CANCELLO MAMBO SAFI

KLABU ya Manchester City inataka kumpatia beki wa Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Cancell, mwenye umri wa miaka 27 mkataba mpya ifikapo mwakani. ***(Fabrizio Romano)***

### MADRID: HAZARD HAONDOKI

OMBI la West Ham kutaka kumsajili mchezaji wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Eden Hazard kwa dau la pauni milioni 21 limekataliwa na Real Madrid. ***(El Nacional)***

### RAPHINA KUTUA LIVERPOOL

LIVERPOOL inawanyatia winga wa Leeds na Brazil, Raphina mwenye umri wa miaka 24, na mshambuliaji wa West Ham, Jarrod Bowen (24), kabla ya kuwasajili katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Liverpool Echo)***

### DYBALA ATAJWA EPL

LIVERPOOL imeweka wazi inamchunguza mshambuliaji wa Juventus na Timu ya Taifa ya Argentina, Paulo Dybala ambaye ana umri wa miaka 28. ***(Calciomercato)***

### XAVI KUIJENGA BARCELONA

KOCHA wa Barcelona, Xavi anatarajiwa kuamua kuhusu usajili wa Januari wa kiungo wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 24, beki wa Marekani, Sergino Dest (21), na kipa wa Ujerumani, Marc-Andre ter Stegen (29), wote wakiwa tayari kuhama timu zao. ***(Gerard Romero, via Sun)***

### BARCA KUMUUZA COUTINHO

BARCELONA pia huenda ikamuuza kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Brazil, Philippe Coutinho mwenye umri wa miaka 29, na beki wa Ufaransa, Samuel Umtiti (28). ***(Sport)***

### ADEYEMI AGOMBEWA ULAYA

KLABU ya Borussia Dortmund wanapigiwa upatu kumsajili mshambuliaji wa Red Bull Salzburg na Ujerumani, Karim Adeyemi mwenye miaka 19, ambaye pia anahusishwa na Bayern Munich na Liverpool. ***(Goal)***

### VINICIUS AICHAGUA MADRID

WINGA wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Brazil, Vinicius Junior mwenye umri wa miaka 21, amesema ana lengo la kutaka kusalia katika klabu hiyo ya LaLiga. ***(Vamos, via Marca)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# TUCHEL ATOA HATIMA YA WERNER, ZIYECHI

Kocha huyo asema nyota hao wako katika mipango kwenye kikosi chake...

**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, ameripotiwa kuweka msimamo wake, si Timo Werner wala Hakim Ziyech atakayeondoka Stamford Bridge wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari.

Barcelona wamehusishwa zaidi na wachezaji hao wote wawili, huku miamba hao wa Katalunya wakiwa wanajaribu kuimarisha safu yao ya ushambuliaji mwanzoni mwa mwaka 2022 kwa usajili wa mkopo.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Sport, Barca inayonolewa na Xavi imefahamishwa hakuna mchezaji wa Chelsea atakayepatikana katika dirisha dogo la Januari.

Taarifa hiyo inadai Tuchel anataka kuwaweka pamoja kuwa sehemu kubwa ya kikosi chake cha kwanza kwa msimu mzima, huku The Blues hao wakipania kuwania taji la Ligi Kuu England na lile la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Werner amefunga mara tatu na kutoa asisti moja kwenye mechi 12 alizoichezea Chelsea msimu huu.

Ziyech, ambaye alihusishwa sana na kutaka kuondoka Stamford Bridge msimu wa joto, amechangia kucheza na nyavu mara tatu na kutoa asisti nne katika mechi 15 za ugenini kwa mashindano yote.

MECHI KALI
HOME
AWAY
NORWICH CITY
6.02 | 4.23 | 1.52
MANCHESTER UTD
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa
halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 761



# BALE SASA AJIPANGA KURUDI TOTTENHAM

**LONDON, England**

KLABU ya Tottenham Hotspur inaripotiwa kutafakari kuungana tena na Gareth Bale katika dirisha dogo la usajili litakalofunguliwa Januari, kwa mujibu wa vyombo vya habari vya England.

Licha ya panda shuka wakati wa mkopo wa msimu mzima huko London Kaskazini msimu wa 2020-21, Bale alichangia mabao 15 na 'asisti' nne.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Wales amerejea katika klabu yake 'mama' ya Real Madrid, ambako amebakiza miezi saba katika mkataba wake na hadi sasa na hakuna taarifa au mipango ya wazi ya kuongezwa mkataba mwingine.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, kipindi cha tatu ndani ya Spurs kinaweza kuwa chaguo pekee ikiwa, Antonio Conte ataidhinisha mpango huo.

Huku wakiwa wanakosa msaada wa Harry Kane, ukiachana na chipukizi, Dane Scarlett, timu hiyo ya Ligi Kuu England inaweza kuingia sokoni kumnunua mchezaji mpya katika safu ya ushambuliaji.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 hajaichezea Real Madrid tangu Agosti, mwaka huu kutokana na changamoto ya jeraha.

# Hakimi ataka kurejea Madrid

**PARIS, Ufaransa**

MLINZI wa Paris Saint-Germain, Achraf Hakimi, ameripotiwa kuwa na nia ya kurejea Real Madrid.

Katika msimu wake wa kwanza akiwa na klabu hiyo ya Parc des Princes, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 amefanikiwa kuingia kwenye kikosi cha kwanza mara kwa mara, akicheza mechi 20 huku akitokea benchi mara mbili kwenye mashindano yote.

Mkataba wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Morocco na mabingwa hao wa Ufaransa unadumu hadi mwaka 2026, na hii inabainisha kuna uwezekano mdogo wa kuhama mwaka 2022.

Hata hivyo, kwa mujibu wa El Nacional, beki huyo wa pembeni mwenye ufundi wa kushambulia anataka kujiunga tena na Los Blancos ikiwa ni mwaka mmoja tu baada ya kuondoka.

Ingawa ripoti hiyo inaonyesha maofisa wa Real Madrid wanafuatilia hali hiyo, lakini hawana uwezekano wa kutaka kufikia bei ambayo walipokea mapema mwaka huu kwa Hakimi.

Hakimi inasemekana gharama yake ni euro milioni 71, dau ambalo pia lilijumuisha nyongeza ambazo zinaweza kukamilishwa katika misimu ijayo.



**HABARI MICHEZO**

,374,640

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/12/21 | 18:00 | Peterborough vs Millwall | 3.04 | 3.19 | 2.29 |
| 02. 11/12/21 | 18:00 | Derby vs Blackpool | 2.34 | 3.14 | 2.99 |
| 03. 11/12/21 | 18:15 | Alaves vs Getafe | 2.37 | 2.94 | 3.34 |
| 04. 11/12/21 | 23:00 | Athletic Bilbao vs Sevilla FC | 2.64 | 3.09 | 2.79 |
| 05. 12/12/21 | 14:30 | Torino vs Bologna | 2.30 | 3.25 | 3.15 |
| 06. 12/12/21 | 15:00 | Lille vs Lyon | 2.50 | 3.49 | 2.65 |
| 07. 12/12/21 | 17:00 | Brighton vs Tottenham | 3.00 | 3.20 | 2.42 |
| 08. 12/12/21 | 17:00 | Metz vs Lorient | 2.35 | 3.28 | 2.99 |
| 09. 12/12/21 | 19:00 | Strasbourg vs Marseille | 2.64 | 3.34 | 2.59 |
| 10. 12/12/21 | 19:30 | Crystal Palace vs Everton | 2.27 | 3.20 | 3.25 |
| 11. 12/12/21 | 20:00 | Sassuolo vs Lazio | 2.89 | 3.49 | 2.34 |
| 12. 12/12/21 | 20:15 | Alcorcon vs FC Cartagena | 2.94 | 2.94 | 2.50 |
| 13. 12/12/21 | 20:30 | Betis vs Real Sociedad | 2.35 | 3.25 | 3.05 |

## MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAMOSI - 11 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2260 | Kryliya Sovetov vs Rubin Kazan | 2.10 | 3.29 | 3.34 |
| 15:30 | 4373 | Thailand vs Myanmar | 1.12 | 6.52 | 18.21 |
| 15:30 | 5054 | Manchester City vs Wolverhampton | 1.19 | 6.44 | 15.66 |
| 16:00 | 3451 | Espanyol vs Levante | 2.04 | 3.34 | 3.69 |
| 16:00 | 4545 | Green Buffaloes vs Buildcon | 1.66 | 3.35 | 6.20 |
| 16:30 | 1647 | Chippa Utd vs Amazulu | 3.00 | 2.70 | 2.65 |
| 17:00 | 5402 | Fiorentina vs Salernitana | 1.32 | 5.22 | 8.83 |
| 17:30 | 1837 | Bayern Munchen vs Mainz | 1.21 | 6.75 | 10.92 |
| 17:30 | 2276 | VfL Bochum vs Borussia Dortmund | 5.38 | 4.68 | 1.50 |
| 17:30 | 3575 | RB Leipzig vs Monchengladbach | 1.74 | 4.08 | 4.08 |
| 17:30 | 4258 | SC Freiburg vs Hoffenheim | 2.38 | 3.49 | 2.79 |
| 17:30 | 4396 | Hertha BSC vs Arminia Bielefeld | 2.03 | 3.25 | 3.79 |
| 18:00 | 1053 | Ross County vs Dundee FC | 2.19 | 3.16 | 3.31 |
| 18:00 | 2417 | Raith Rovers vs Kilmarnock | 2.74 | 3.13 | 2.50 |
| 18:00 | 2909 | Swansea vs Nottingham | 2.16 | 3.20 | 3.30 |
| 18:00 | 3065 | Derby vs Blackpool | 2.34 | 3.09 | 3.04 |
| 18:00 | 3160 | Dundee Utd vs Livingston | 2.32 | 3.06 | 3.16 |
| 18:00 | 3916 | Preston vs Barnsley | 1.80 | 3.43 | 4.32 |
| 18:00 | 3942 | Peterborough vs Millwall | 3.04 | 3.19 | 2.29 |
| 18:00 | 4380 | Arsenal vs Southampton | 1.71 | 3.82 | 4.68 |
| 18:00 | 4398 | Liverpool vs Aston Villa | 1.24 | 6.63 | 10.04 |
| 18:00 | 5470 | Luton Town vs Fulham | 3.79 | 3.59 | 1.86 |
| 18:00 | 5568 | Hull City vs Bristol City | 2.06 | 3.30 | 3.44 |
| 18:00 | 5677 | Birmingham vs Cardiff | 2.31 | 3.19 | 3.00 |
| 18:00 | 5787 | Stoke City vs Middlesbrough | 2.34 | 3.14 | 2.99 |
| 18:00 | 5855 | Bournemouth vs Blackburn | 1.70 | 3.69 | 4.52 |
| 18:15 | 2571 | Panathinaikos vs Atromitos | 1.42 | 4.34 | 7.10 |
| 18:15 | 3722 | Alaves vs Getafe | 2.46 | 2.90 | 3.25 |
| 18:30 | 5155 | Orlando Pirates vs TS Galaxy FC | 1.67 | 3.40 | 5.32 |
| 18:30 | 5596 | Maritimo vs Santa Clara | 2.50 | 3.04 | 2.89 |
| 19:00 | 1008 | Josko Ried vs SCR Altach | 1.97 | 3.37 | 3.37 |
| 19:00 | 1319 | RB Salzburg vs WSG Wattens | 1.13 | 7.31 | 13.46 |
| 19:00 | 3163 | Rostov vs Ural Yekaterinburg | 1.95 | 3.28 | 3.82 |
| 20:00 | 1051 | Venezia vs Juventus | 6.94 | 4.40 | 1.45 |
| 20:00 | 1177 | FC Schaffhausen vs FC Stade LS Ouchy | 2.01 | 3.47 | 3.18 |
| 20:00 | 1315 | FC Wil vs FC Winterthur | 2.80 | 3.33 | 2.26 |
| 20:00 | 4640 | Lausanne vs Sport-FC Zurich | 3.11 | 3.56 | 2.12 |
| 20:30 | 1741 | VfL Wolfsburg vs Stuttgart | 1.82 | 3.68 | 4.08 |
| 20:30 | 4061 | Valencia vs Elche | 1.75 | 3.59 | 4.79 |
| 20:30 | 5715 | Norwich City vs Manchester Utd | 6.02 | 4.23 | 1.52 |
| 20:45 | 1851 | Utrecht vs GO Ahead Eagles | 1.38 | 4.81 | 6.68 |
| 22:00 | 2949 | Lechia Gdansk vs Jagiellonia | 1.85 | 3.43 | 3.72 |
| 22:00 | 4831 | Heerenveen vs Sparta Rotterdam | 2.03 | 3.43 | 3.38 |
| 22:30 | 5636 | St. Gallen vs FC Lugano | 2.45 | 3.36 | 2.71 |
| 22:45 | 1170 | RFC Seraing vs Anderlecht | 5.12 | 4.23 | 1.55 |
| 22:45 | 3545 | Udinese vs AC Milan | 4.01 | 3.56 | 1.89 |
| 23:00 | 1855 | Reims vs St Etienne | 2.17 | 3.19 | 3.44 |
| 23:00 | 5125 | Athletic Bilbao vs Sevilla FC | 2.50 | 3.05 | 3.00 |
| 23:00 | 5794 | PEC Zwolle vs Fortuna Sittard | 1.78 | 3.63 | 4.13 |
| 23:30 | 4249 | Sporting Lisbon vs Boavista | 1.18 | 6.53 | 13.85 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SIMBA QUEENS, YANGA PRINCESS KUVAANA JAN. 8

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi, Simba Queens watakutana na watani zao, Yanga Princess katika mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania itakayochezwa Januari 8, mwaka huu kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Pazia rasmi za ligi hiyo litafunguliwa ifikapo Desemba 23, mwaka huu kwenye viwanja mbalimbali hapa nchini.

Kwa mujibu wa ratiba ya ligi hiyo iliyotolewa jana inasema Simba Queens wataanza kampeni ya kutetea ubingwa wanaoushikilia nyumbani dhidi ya Ruvuma Queens kwenye Uwanja wa Mo Simba Arena ulioko Bunju jijini.

Mechi nyingine itakayochezwa siku hiyo itakuwa ni Alliance Girls watakao wakaribisha Mlandizi Queens kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza huku Desemba 24, mwaka huu JKT Queens watawakabili Oysterbay Girls kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo uliopo Mbweni na TSC Queens watawavaa Tigers Queens kwenye dimba la CCM Kirumba, Mwanza.

Fountain Gate Princess watakuwa nyumbani kuwakaribisha Ilala Queens, Uwanja wa Fountain Arena uliopo jijini Dodoma huku Baobab Queens itawaalika Yanga Princess kwenye Uwanja wa Jamhuri.

Desemba 27, mwaka huu kutakuwa na mchezo mmoja kati ya Alliance Girls dhidi ya The Tigers Queens na siku inayofuata Fountain Gate Princess watacheza dhidi ya Yanga Princess, Uwanja wa Fountain Arena, Simba Queens wakaivaa Oysterbay Girls na Desemba 28, mwaka huu Baobab Queens watawakaribisha Ilala Queens huku JKT Queens wakiwaalika Ruvuma Queens.



Wachezaji wa Simba Queens wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania itakayofanyika kuanzia Desemba 23, mwaka huu. Simba Queens ndio mabingwa watetezi wa ligi hiyo. **PICHA: SIMBA SC**

# Azam kuongeza wawili wapya

**Na Dennis Fussi**

OFISA Mtendaji Mkuu wa Azam, Abdulkarim Amin 'Popat' amesema klabu hiyo ina mpango wa kusajili wachezaji wapya wawili hadi watatu kwenye dirisha dogo la usajili.

Hata hivyo, hali hiyo itategemea na uhitaji wa benchi la ufundi lililopo chini ya Mzambia George Lwandamina.

Popat amesema pamoja na timu yao kuanza msimu kwa kusuasua, lakini bado wana imani na uwezo wa wachezaji wao ikizingatiwa ligi bado ni ndefu.

"Hatujafanya vibaya sana sababu ndiyo kwanza tumecheza mechi saba, hatupo mbali sana na timu inayoongoza ligi," alisema Popat.

Kiongozi huyo alisema; "Kwa sasa tunawasikiliza benchi la ufundi kama litahitaji kuongeza nguvu tutafanya hivyo."

Azam inashika nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara ikiwa na pointi 10 katika mechi saba ilizocheza ambapo imepoteza tatu, kushinda tatu na kwenda sare mchezo mmoja.

Michezo

Jumamosi Desemba 11, 2021

Nipashe



Tuchel atoa hatima ya Werner, Ziyechi

# SIMBA, YANGA 'KITAUMANA'

## ●●●Muda umefika wa kumaliza ubishi na majigambo ya vigogo hao...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

KWA mara nyingine Afrika Mashariki na Kati inatarajia kusimama kwa dakika 90 ili kupisha 'dabi' kubwa zaidi kwenye ukanda huu, Simba na Yanga zitakapokutana katika mechi ya mzunguko wa kwanza ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Mechi hiyo itachezwa kuanzia saa 11:00 jioni chini ya mwamuzi wa kimataifa, Herry Sasii ambaye atasaidiana na Kassim Mpanga na Hamdani Saidi wakati mwamuzi wa mezani atakuwa ni Ahmada Simba.

Hii itakuwa ni mechi ya 102 ya Ligi Kuu tangu timu hizo zilipoanza kucheza ligi hiyo mwaka 1965 na kuingia kwenye vitabu vya kumbukumbu za mapambano hayo.

Mpaka sasa Yanga inayotumia jezi za rangi ya kijani na njano imeshinda mara 39 na Simba wanaovaa jezi nyekundu na nyeupe wakishinda mara 31 na sare mara 31 pia.

Mechi hii ya mzunguko wa kwanza ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara kwa msimu wa 2021/22, Simba ndiyo mwenyeji wa mechi ya leo, itaingia ikiwa na kumbukumbu ya kupoteza mechi ya Ngao ya Jamii kwa bao 1-0, iliyochezwa Septemba 25, mwaka huu shukrani kwa Fiston Mayele, ambaye alifunga bao hilo pekee.

Msimu uliopita wa 2020/21, timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1 kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza, Yanga ikipata bao lake kupitia kwa Michael Sapong kwa njia ya penalti na Simba ikasawazisha dakika za lala salama kupitia kwa beki Mkenya, Joash Onyango, mechi ikichezwa Novemba 11, 2020.

Mechi ya mzunguko wa pili ilikuwa ni Julai 3, mwaka huu, Yanga ilishinda bao 1-0 lililofungwa na Zawadi Mauya.

Itakuwa ni kwa mara ya kwanza, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, raia wa Hispania kukiongoza kikosi hicho kwenye 'dabi' tangu ajiunge na timu hiyo mwezi uliopita lakini kwa Nasreddine Nabi, wa Yanga yeye itakuwa ni mara ya pili kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.



Kocha Nabi

Nabi aliiongoza timu hiyo kwenye mechi ambayo Yanga ilishinda bao 1-0 kwa bao la Mauya, achilia mbali mechi ya Ngao ya Jamii na ile ya Kombe la FA iliyochezwa Julai 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma na kulala kwa goli 1-0, mfungaji akiwa ni Thadeo Lwanga.

Katika mechi ya leo, Simba itawategemea zaidi, Aishi Manula, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr', Meddie Kagere, Mzamiru Yassin, Jonas Mkude, lakini pia ina 'hazina' ya wachezaji wawili wapya, Israel Mwenda na Kibu Dennis ambao tayari wameanza kuaminika kwenye kikosi cha kwanza cha timu hiyo.

Mwenda alisajiliwa Simba msimu huu akitokea KMC ya Dar es Salaam na Kibu ambaye uraia wake uligubikwa na utata ametokea Mbeya City.

Akizungumza jana jijini, Nabi alisema mchezo wa 'dabi' ni mkubwa kwake na kikosi chake kimejiandaa vizuri kuelekea mchezo huo kwa kupata matokeo mazuri ambayo yatawasaidia kujiweka katika nafasi nzuri ya kufikia malengo yao.

Nabi alisema amewataka wachezaji wake kuweka pembeni mitandao ya kijamii na akili zao kuelekeza katika mchezo huo kwa kujipanga kupambana kutafuta matokeo chanya.

"Kisaikolojia wachezaji wangu nimewatengeneza vizuri, tunatambua Simba ni timu nzuri na tunaiheshimu, hatuwezi kujiaminisha kwamba tuko bora zaidi na kwenda uwanjani kwa kujiamini.

"Kila mechi ina kanuni zake na mbinu za uwanjani, mbali na ufundi tunaowapa wachezaji wetu, kuhusu mechi ya 'dabi' inaweza kuwa 50/50 yoyote anaweza kushinda kutokana na maandalizi lakini pia wachezaji watakavyoyapokea na kufanyia kazi maelekezo," alisema Nabi.

Kuhusu mabadiliko ya benchi la ufundi kwenye kikosi cha watani zao, Nabi alisema anamkaribisha Tanzania, Pablo Franco, na kumweleza ni nchi ambayo watu wake wanapenda mpira na anajua mabadiliko hayo hayawezi kuwavuruga.

"Makocha hawachezi, bali tunaifahamu Simba, wataingia kwa mbinu gani, watacheza vipi na watajua wanaingia na mfumo gani ili kupata matokeo," alisema Nabi.



Kocha Pablo

Yanga katika mechi hiyo inawategemea nyota wake mbalimbali wakiongozwa na golikipa, Diara, Mayele, Jesus Moloko, Khalid Aucho na mkongwe, Saido Ntibazonkiza.

Simba, wawakilishi pekee wa nchi waliobakia katika mashindano ya kimataifa watashuka dimbani katika mchezo huo wakiwa na kumbukumbu ya kutinga hatua ya makundi ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa ushindi wa jumla ya mabao 4-2 dhidi ya Red Arrows ya Zambia huku Yanga wao walipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Mbeya Kwanza, kwenye mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara iliyochezwa Desemba 01, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sokoine, Mbeya.

Yanga ndio vinara wa ligi hiyo wakiwa na pointi 19 huku Simba ikiwa nafasi ya pili baada ya kujikusanyia pointi 17, timu zote zimecheza mechi saba.

**SIMBA YAANZA MGOMO**

Siku chache baada ya kuandika barua kwa Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), kuomba ufafanuzi kuhusiana na mkataba mpya wa kudhamini ligi uliosainiwa kati ya Shirikisho la Soka Nchini (TFF), na Kampuni ya GSM, uongozi wa Simba ulimzuia kocha wake, Pablo kushiriki katika kikao cha maandalizi kuelekea dabi hiyo.

Simba ilitoa maelekezo hayo kutokana na kuwapo kwa bango la GSM ambaye ni mdhamini mweza wa ligi hiyo ya juu Tanzania Bara.

Ofisa Mtendaji Mkuu, Barbara Gonzalez, alikuwapo katika ofisi za TFF akiwaongoza watendaji wengine wa Simba akiwamo Kaimu Ofisa Habari, Ally Shatry ambaye alihitaji kuondolewa bango la GSM ili washiriki mkutano huo.

Mapema wiki hii, Simba ilitoa taarifa ikisema haiko tayari kuvaa nembo ya GSM mpaka pale itakapopata ufafanuzi kuhusiana na mkataba huo na iko tayari kulipa faini kwa kugomea kuvaa nembo hiyo ya mdhamini mwenza.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >